

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 12 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 234

**Kuwafuta Machozi Wananchi Walioathirika na Vurugu za Uchaguzi Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Wakazi wa Liwale waliathirika na vurugu za Uchaguzi wa mwaka 2020 na mali za wananchi na Serikali zilichomwa moto:-

Je, Serikali kupitia Mfuko wa Maafa ina mpango gani wa kuwafuta machozi wananchi walioathirika na vurugu hizo?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri kupata taarifa za kutokea kwa vurugu zilizosababishwa na wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na kuleta uvunjifu wa amani, uharibifu wa vitu mbalimbali ikiwemo mali za wananchi na Serikali. Uhalifu huo umefanyika wakati wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 katika Jimbo la Liwale na

maeneo mengine Mkoani Lindi. Aidha, Serikali ilifanya jitihada mbalimbali za kumaliza vurugu hizo kwa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, kufanya vurugu za aina hii ni kosa la jinai. Hivyo, matokeo ya madhara ya vurugu hizo yatahughulikiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusu masuala ya makosa ya jinai. Sheria ambayo inahusika kwenye masuala ya makosa ya jinai ni Sheria ya Kanuni za Adhabu (*Penal Code CAP.16*) ambayo imefanyiwa marekebisho mara kwa mara, lakini kwa Sheria ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2015 na Kanuni zake za utekelezaji hazina ufungamanisho wa pamoja na madai ya kijinai na hasa yahusuyo uharibifu wa mali na namna ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapa pole sana wananchi wote walioathirika na kadhia hii kwa sababu si jambo zuri. Serikali pia ililipokea na kulifanyia kazi lakini tunatambua kwamba kuna uharibifu wa nyumba ambao ulifanyika, kuna uharibifu wa mali kama magari, pikipiki na vifaa vinginevyo ambapo hata timu ya mkoa tayari ilikwishakuanza kuchukua hatua za awali za kufanya tathmini ya kujua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Lindi kuhakikisha uchunguzi kuhusu vurugu hizo unakamilika na hivyo kulifikisha suala hilo katika vyombo vya sheria ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuwapa pole wale wote walioathirika na vurugu hizo na kuwaomba wananchi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kudumisha amani na usalama nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali ambayo naweza kusema kwamba hayaridhishi. Kwanza ni-*declare interest* kwamba na mimi ni miongoni mwa waathirika, nimepoteza mali yenye thamani ya zaidi ya shilingi 301,516,000. Pia kuna nyumba zaidi ya sita zenye thamani ya shilingi 417,300,000; magari nane yenye thamani ya shilingi 299,700,000; pikipiki nane zenye thamani ya shilingi 22,100,000 na vifaa vya ndani vyenye thamani ya zaidi ya shilingi 145,169,000. Jumla uharibifu huu umeigharimu halmashauri yetu zaidi ya shilingi milioni 886.

Mheshimiwa Naibu Spika, waathirika, kama nilivyosema, mimi mwenyewe ni mmoja wao, lakini yuko Musa Mkoyage, Hassan Liwango...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, hilo ni swali, uliza swali lako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Sasa swali langu; hivi ni kweli Serikali pamoja na uharibifu huu mkubwa haioni umuhimu wa wananchi hawa waathirika zaidi ya 15 angalau kuwashika mkono? Ni kweli nchi yetu inaongozwa kwa sheria pamoja na kanuni, lakini kuna mila na desturi ya kufikiria kwamba hawa watu wameathirika, hawana mahali pa kuishi, hawana namna nyingine yoyote ya kushiriki maendeleo ya nchi hii; kweli Serikali haioni umuhimu wa kuwashika mkono watu hawa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiri kwamba jambo lililofanyika siyo zuri na Serikali imelipokea kwa uchungu mkubwa. Kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema vizuri ni kwamba ni kweli nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria

na sheria inayoongoza hapa ni Sheria ya Menejimenti ya Masuala ya Maafa ambayo ni ya mwaka 2015, yanapogeuka kuwa makosa ya jinai tayari inakuwa imeingia katika utaratibu mwingine. Ukisema ulipe fidia kwa watu ambao wamefanya uharibifu wa maji, kwa mfano, *squandering of property*, lakini pia kunakuwa na *overt act* kwa maana ya tendo ovu ambalo limekusudiwa, sasa tunaangalia ile *mens rea* na *actus reus*; kama tendo limefanyika ambalo kimsingi limevunja sheria maana yake hatua kali za kisheria lazima zichukuliwe kwa sababu ukilipa fidia kwa watu ambao wamefanya makosa maana yake tunachochea zaidi watu wengine kuleta madhara zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Amiri Jeshi Mkuu na vyombo vyake vya ulinzi na usalama wakati wa uchaguzi au maafa lakini pia wakati wa sherehe zote za Kitaifa na nyakati zote kuna timu ambazo zimeandaliwa, kuanzia ngazi ya kata tunazo kamati ambazo zinahusika na kufanya upembuzi wa kujua kwamba hili ni janga na ni afa ambalo linahitaji kuweza kuingia katika *perimeters* za Sheria hii ya Menejimenti ya Masuala ya Maafa. Pia kwenye ngazi ya wilaya, tunao Wakuu wa Wilaya ambao wanaongoza Kamati za Ulinzi na Usalama, ambazo ndizo timu pia za maafa kwa ajili ya kufanya ile *assessment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa suala hili lilivyojitokeza Liwale, moja kwa moja ni kosa la jinai. Kwa hiyo, hatua zitachukuliwa na kwa hatua ya sasa tayari *evaluation* imefanyika, nadhani tumeshauriana ameliona hilo, ni jinsi ambavyo tunataka sasa kuja kupata taarifa ya mwisho ya jinsi gani ambavyo madhara yalifanyika, watuhumiwa waliokamatwa na hatua kuchukuliwa zaidi ili kuweza kupeleka kesi zenye ushahidi mahakamani ili waweze kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kusisitiza wananchi wote kufuata sheria, taratibu na kanuni katika maeneo yao. Niseme tu hili, imekuwa ikijitokeza mara nyingi kwenye uchaguzi, watu wanaposhindwa hawakubali kwamba wameshindwa matokeo yake anataka kufanya

*justification* ya kutaka kuonesha kwamba yeye alikuwa na nguvu kwa hiyo wanatengeneza matukio ya kihalifu. Kumekuwa na timu ambazo wanaleta vijana kwa ajili ya kufanya uhalifu huo. Serikali iko imara, vyombo vya ulinzi na usalama viko imara, navipongeza kwa hatua ambazo wamekwishaanza kuzichukua na ambazo tunaendelea nazo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kupongeza Jeshi letu la Polisi katika kipindi cha uchaguzi limefanya kazi nzuri. Nipongeze Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, hata kwenye maafa haya lilihusika. Nipongeze pia vijana wa *Scout* lakini pia vijana wetu wa *Red Cross* ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunakwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 235

### **Ujenzi wa Barabara ya Makanya Hadi Machimbo ya Jasi**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Makanya kwenda kwenye Machimbo ya Jasi Wilayani Same?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali

Ia Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makanya hadi kwenye Machimbo ya Jasi Wilayani Same ina urefu wa kilometa 40.9. Kipande cha kilometa 4.5 cha barabara hii kimeinuliwa kwa kujengwa tuta kati ya kilometa 14.5 zinazotakiwa kujengewa tuta kwa kiwango cha changarawe. Kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kuwa barabara hii inapitika muda wote na ndiyo maana imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara.

Katika mwaka wa fedha 2021/2020, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) Wilaya ya Same umefanya matengenezo ya barabara ya Makanya hadi kwenye Machimbo ya Jasi maeneo korofi yenye urefu wa kilometa 3.54 kwa gharama ya shilingi milioni 77.36.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Same imefanya matengenezo ya barabara hiyo kipande chenye urefu wa kilometa mbili kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 49.4. Vilevile katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 61.25 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe yenye urefu wa kilometa moja pamoja na ujenzi wa makalavati 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Makanya hadi kwenye Machimbo ya Jasi na itaendelea kuifanyia matengenezo ili kuhakikisha inapitika. Serikali itatoa kipaumbele cha ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika bajeti zijazo ili kuiboresha na kurahisisha usafirishaji wa Jasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni ukweli usiopingika kwamba ni barabara ambayo haipitiki kipindi chote cha mvua. Ni barabara ambayo inaleta manufaa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa madini ya jasi ya Makanya yanalisha viwanda vya *Tanga Cement, Twiga Cement, Moshi Cement*, Doria Arusha na nchi za Rwanda na Burundi na kuingizia Serikali mapato. Serikali haioni haja ya kuiboresha barabara kwa kuitengea fedha ili iweze kufanya kazi muda wote na kuongeza mapato ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, katika machimbo haya wako wanawake ambao wamewekeza kule ambao wamepata fursa ya kuendesha biashara ya mama lishe na biashara ndogondogo. Je, Serikali haioni kwamba kwa kusimama kwa machimbo haya kutokana na barabara korofi wanawake hawa wanadhooifika kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza maswali mawili ya msingi kabisa ambayo yana nia njema ya kuwasaidia wanawake wote wa Same mpaka Mkoa mzima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza la msingi ambalo ameuliza hapa, amesema barabara hii haipitiki na ameomba Serikali tutenge fedha. Kwa kuwa maombi haya yametoka kwa mtu ambaye ameshakuwa kiongozi ndani ya chama na ni maombi muhimu sana,



nimwambie tu kwamba tutatuma wataalam wetu wa Ofisi ya Rais, *TARURA*, waende katika eneo hilo wakafanye tathmini ya kina na kuileta ofisini ili tuone namna ambavyo tunaweza tukasaidia barabara hii iweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amesema kwamba kusimama kwa machimbo ya jasi kunasababisha uchumi kwa akina mama kuyumba na kuomba watu wa Ofisi ya Rais, *TAMISEMI* kusaidia ili barabara hiyo iweze kujengwa. Kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba tutahakikisha barabara hiyo inatengenezwa na inapitika kwa wakati wote kuhakikisha tunasaidia akina mama hao wanaoendesha biashara zao maeneo yale lakini vilevile tunawasaidia wananchi wa Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika majibu ya msingi, Naibu Waziri ametueleza kwamba kwa kipindi kifupi Serikali imewekeza pale takribani shilingi milioni 130 hivi kwa kuweka changarawe na kukarabati. Hata hivyo, kila baada ya ukarabati huo, mvua ikija inazoa changarawe zile na shida inabakia palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shida ambazo mwenye swali alishazizungumzia, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuanza kuweka lami katika kilometa chache chache ili shida hiyo ya kupoteza hela za Serikali iishe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, *TAMISEMI*, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba tunatuma wataalam wa *TARURA* pale wakafanye tathmini na baada ya tathmini hiyo wata kayotuletea ndiyo tutafanya maamuzi ya kwamba sasa ijengwe hilo lami kama ambavyo nilimjibu mwenye swali la msingi, ama tuweke kiwango cha changarawe. Kitu ambacho nina uhakika nacho ni kwamba Serikali yetu ni makini na inasikia, lengo lake ni kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa wakati wote. Ahadi zetu siyo za uongo, tuko hapa kwa ajili ya kufanya kazi na tutahakikisha barabara hiyo inapitika wakati wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa akina mama wa Jimbo la Same Magharibi wengi wao nao pia wako katika Machimbo haya ya Jasi na wanachimba jasi kwelikweli. Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu hawa akina mama kupata mikopo maalum kwa sababu uchimbaji wa jasi unatumia pesa nyingi? Kama inawezakana, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwapa mikopo akina mama wote wa Tanzania ambao wanachimba madini? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, Serikali ni moja, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali la msingi lilikuwa linataka tujenge barabara tuwasaidie, lakini miongoni mwa majibu ambayo tulikuwa tumetoa ni pamoja na kuwainua akina mama ambao wanafanya kazi katika machimbo hayo ya jasi.

Mheshimiwa Mbunge wa Same Mashariki amependekeza Serikali itenge fedha kwa ajili ya kupeleka mikopo na sisi sasa hivi katika moja ya sheria ambazo tulipitisha ndani ya Bunge ni kuhakikisha zile asilimia kumi za mikopo kutokana na mapato ya ndani zinakwenda katika hayo makundi ya akina mama, vijana na watu wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumelipokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na nafikiri moja ya kipaumbele ambacho tutakizingatia ni hicho. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde kwa majibu mazuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde kwa majibu mazuri. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Mama Anne Kilango, ame-raise humu ndani hoja ya msingi sana ya kutambua makundi maalum na hasa ya wanawake yenye mahitaji maalum ya mikopo kwa ajili ya shughuli za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mama Anne Kilango, pia niwatangazie na Wabunge wengine wote, kupitia mpango maalum wa Serikali, tayari tumeanzisha mfuko maalum wa *SUNVIN*; tunauita hivyo kwa ajili ya ku-*support* shughuli hizi za akina mama na

wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kuji-*transform* na kufanya biashara kubwa na hasa za uwekezaji kwenye viwanda, madini na shughuli nyingine zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kuwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili mpate taarifa ya mfuko huo akina mama na Watanzania wengine waweze kuanza kuutumia. Tayari mfuko huo umeshakuwa na fedha na umeshaanza kutumika kufanya uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali nchini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali ilivyo katika eneo la Makanya huko Same inafanana moja kwa moja na hali ilivyo katika Kata za Mwabomba na Mwandu katika Jimbo la Sumve, ambapo barabara za kutokea Mwabomba kupitia Chamva - Mulula mpaka Manawa hazipitiki katika kipindi chote cha mvua:-

Je, lini sasa Serikali itaamua kuzijenga kwa kiwango barabara hizi ili ziweze kupitika katika mwaka wote ili watu hawa waweze kufanya shughuli zao za maendeleo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni amesainisha maeneo ya Kata kadhaa, kama nne hapa ambazo hazipitiki kabisa. Nami tu niwaagize *TARURA* Makao Makuu, ninaamini hapa wananisikiliza, wakafanye tathmini kama ambavyo nimeagiza katika eneo la Same ili walete hiyo taarifa. Kwa sababu sasa hivi tunahitaji tathmini za kina ili tuhakikishe hizi barabara tusiwe tunazungumza tu hapa, tunaleta maneno maneno. Tuzungumze kwa *data* na

tuhakikishe kabisa kila barabara, hususan zile ambazo hazipitiki kabisa tunazitengea fedha na kila fedha inayopatikana inajenga ili kuhakikisha barabara zote zinapitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nilichukue hilo jambo na tayari nimeshaagiza sasa hivi, watafanya tathmini na nitaleta majibu kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita, sasa aulize swali lake.

Na. 236

### **Barabara Zinazohudumiwa na TARURA – Jimbo La Geita**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara za kutoka Rubanga – Isulwabutundwe – Mkoba -Kukuruma – Kamhanga - Kishinda na Mkolani zitatengewa fedha na *TARURA* kwa ajili ya ujenzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyotajwa vinaunganishwa na barabara za *Mkoba Bridge* – Isulwabutundwe – Lubanga yenye urefu wa kilometa 15 na Geita – Isamilo – Mkolani kwa maana ya Busekeseke yenye

urefu wa kilometa 18 ni barabara muhimu sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 barabara hizi zimetengewa jumla ya fedha shilingi milioni 318.83 kwa ajili ya matengenezo ya kilometa 33 na wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa kazi. Kazi zinatarajiwa kukamilishwa mwezi Julai mwaka, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zote zilizo Wilaya ya Geita Vijijini kwa kulingana na upatikanji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wananchi wa Isulwabutundwe, Dubanga, Isamilo, Mkolani, Busekeseke ni wananchi wavumilivu sana. Barabara hizi hazijalimwa kwa miaka 10 sasa; na tunaishukuru Serikali tumepata kiasi cha shilingi milioni 580 kwa ajili ya kulima kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hizi, barabara ya Isamilo - Mkolani – Busekeseke ina urefu wa kilometa 18, tumepata *morum* kilometa 7; hii nyingine ya Mkoba *Bridge* – Isulwabutundwe – Mkolani – Dubanga tumepata kilometa tano. Sasa Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kuuliza: Serikali haioni umuhimu wa kuweza kuongeza fedha kwa dharura ili kipande kilichobaki kuwekewa *moorum* kilimwe kwa pamoja, maana kukilima nusu kitaondoka, halafu tena mwakani tutaanza upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wananchi wa Nyamikoma kupitia daraja la Kimilawinga, daraja hili

inaponyesha mvua halipitiki kabisa na wananchi hawa ni lazima wapite Kimilawinga waende Lwenge, waende Kamwanga kwa ajili ya kupata mahitaji na mpaka Nzela:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga pesa sasa kwa ajili ya kwenda kujenga daraja hili kwa dharura? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza dogo ambalo aliuliza Mheshimiwa Kasheku Musukuma ni kutaka Serikali iongeze fedha katika zile barabara tulizozitoa ili kuhakikisha yale maeneo ambayo *Moorum* haijawekwa, basi yawekwe na yalimwe kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimjibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha huu unaokuja, kuna fedha vile vile imetengwa kwa maana ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya barabara hizo. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba zimepelekewa fedha na itafanya kazi kwa mwaka wa fedha unaokuja kwa sababu huu mwaka sasa tunaamalizia na ndiyo kazi ambazo zinazoendelea kwa wakati uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amezungumzia daraja linalopita Kinilawinga na amehitaji kwamba Serikali ilijenge kwa dharura. Nafikiri suala la madaraja siku zote, ninyi wote hapa mnatambua kabisa kwamba daraja linahitaji tathmini kwanza, baada ya tathmini ndiyo ujue gharama yake ni kiasi gani? Kwa hiyo, niagize tu *TARURA* wakafanye tathmini katika eneo hilo halafu walete Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mremi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kufuatia mvua nyingi ambazo zimenyesha katika Jimbo la Serengeti, barabara nyingi zilizo chini ya *TARURA* sasa zimeharibika sana ikiwemo barabara ya kwenda Iselele, barabara ya kwenda Mosongo lakini pia barabara ya kuzunguka stendi ile. Pia barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami kuzunguka soko la Mji wa Mugumu nayo haijajengwa muda mrefu:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hizi na zile za kufanyiwa marekebisho? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, ameanisha barabara kadhaa ambazo zinahitajika zitengenezwe; na kwa kuwa nafahamu changamoto za barabara kama ambavyo Wabunge wamekuwa waki-*debate* humu ndani ya Bunge; niseme tu, jambo hilo tumelipokea na sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika ule mchakato wetu wa pamoja, tunaandaa *plan* ambayo itahakikisha barabara zote nchini tunazipitia, tunafanya tathmini ya kutosha na kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha hizo barabara zinatengenezwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, awaambie tu wananchi wa Serengeti wakae mkao wa kula, hizi barabara tutazifanyia kazi na kazi yake mtaiona kabla ya miaka hii mitano kwisha. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna umuhimu sana katika barabara ya Singida – Supuka – Ndago ambayo kimsingi inapita katika Jimbo la Waziri wa Fedha pia.



Je, ni lini sasa Serikali itaichimba angalau kwa kiwango cha changarawe barabara hii ambayo zaidi ya miaka kumi haijafanyiwa marekebishi yoyote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge ameuliza barabara ya Supuka – Ndago ambako ni Jimbo la Iramba Magharibi ambapo anatokea Waziri wa Fedha wa sasa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Niseme tu kabisa kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masache, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Nami pia niungane na swali la msingi kama ilivyo Wilaya ya Geita Mjini, kulikuwa na matatizo ya barabara zilizo chini ya *TARURA*. Wilaya yetu ya Chunya pia ina matatizo mengi ya barabara zilizo chini ya *TARURA* zilizoharibika vibaya kutokana na mvua zilizonyesha mwaka huu.

Mheshimwa Naibu Spika, barabara ya kuanzia Lupa kwenda Nkunungu – Lupa - Lwalaje zimeharibika vibaya na kwenye fedha zilizokuwa zimetengwa, zilitengwa maeneo korofi:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za dharura ili barabara hizo ziwewe kutengenezwa ikizingatiwa kuwa maeneo haya zinalimwa Tumbaku na msimu wa soko la Tumbaku unaanza wiki ijayo kwa hiyo, itashindwa kutoka kule? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Masache ameanisha baadhi ya barabara ambazo zimeharibika sana wakati wa mvua yakiwemo madaraja; na sehemu ya hizo barabara *TARURA* walipeleka fedha kwa ajili ya kutatua hizo changamoto za udharura kwa maana ya uharibifu wa hizo barabara. Sasa hivi ameomba tu kwamba Serikali ni lini tutatenga fedha kuhakikisha hizo barabara zinapitika?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la msingi ni kwamba kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyokuwa tutazitengeneza na bahati nzuri maeneo hayo mimi nayafahamu na nimeahidi kufika kujionea mwenyewe hali halisi. Nitakwenda na Mheshimiwa Mbunge na tutazungumza na wananchi. Ninaamini kabisa kwamba kutokana na bajeti ambayo Bunge lilipiga kelele na Serikali ikaongeza, tutafikia maeneo mengi sana mwaka huu wa fedha kuhakikisha tunapunguza hizo changamoto ambazo zinawakabili wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 237

**Ujenzi wa Barabara ya Bulamba hadi  
Masonga - Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Bulamba – Bukonyo hadi Masonga yenye urefu wa kilometa 32.23 kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri ya Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bulamba – Bukonyo hadi Masonga yenye urefu wa kilometa 32.23 ni barabara ya mkoa inayounganisha mji wa Nansio na Ziwa Viktoria kupitia vijiji vya Murutunguru - Bukonyo hadi Masonga. Barabara hii inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inaendelea kuiimarisha kwa kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka ili kuhakikisha kuwa inapatika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 757.94 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii. Kazi za matengenezo hayo inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya barabara hii kila mwaka ili kuhakikisha kuwa inaendelea kupitika wakati wote kabla ya kuijenga kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka ujao wa fedha wa 2021/2022, barabara hii imeombewa shilingi milioni 219.159 kwa ajili ya matengenezo ya vipindi maalum na shilingi milioni 510 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya Daraja la Nabili lililopo katika barabara hiyo. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa

Ukerewe, inasaidia wananchi wanaoenda Kivuko cha Bugorora kwenda Ukara ambako kuna hospitali mpya sasa ya Wilaya ya Bwisya; barabara hii inasaidia wananchi wanaoenda Kakukuru ambapo ndiyo msingi wa uchumi wa Ukerewe, pia inasaidia wananchi wanaoenda Mliti mpaka Luby kwenye msitu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizi za matengenezo ya kawaida zinazotengwa zimekuwa hazisaidii sana kwa sababu inakuwa nzuri kwa muda mfupi, lakini inakuwa haipitiki kwa muda mrefu. Ni kwa nini sasa Serikali isianze kuifanyia Barabara hii upembuzi na hatimaye upembuzi yakinifu ili hatimaye sasa ianze kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo kimsingi siyo swali, ni ushauri; kwenye Kivuko cha Bugolola kwenda Ukara kumekuwa na shida ya kivuko kile na inaweza kusababisha ajali hata gari kutumbukia majini. Kinachohitajika ni kuweka *Moorum* au *trip* kadhaa za mawe ili kutengeneza *gati* lile ili wananchi waweze kuvuka kwa usalama. Kwa hiyo, nitoe ushauri kwa Wizara, kwa haraka na kwa dharura, ifanye kazi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali lake la kwanza Mheshimiwa Mkundi ameomba barabara yake hii ifanyiwe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe Mkundi kwamba tumepokea ombi, tutalifanyia kazi ili tufanye tathimini ya kina halafu tuweze kujua gharama ambayo inahitajika kuwekwa kiwango cha lami ili barabara iweze kutengenezwa na kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili tumepokea ushauri ambao naomba nimwelekeze Mkurugenzi wa vivuko Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwa kuwa amesema kuna hali hatarishi ya maisha katika eneo hili, afanye tathmini, aangalie hali halisi, halafu tuweze kuchukua hatua ya dharura ili kuweza kuokoa maisha ya watu wetu katika eneo hili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali dogo la nyongeza. Naomba kuuliza, Serikali iliahidi kutangaza *tender* ya ujenzi wa barabara ya Gigwa – Kisaki.

Je, ni lini Serikali itatangaza barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kwamba kwa sasa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ipo kwenye hatua mbalimbali za kutangaza baadhi ya barabara ili ziweze kujengwa kwa hatua mbalimbali, nyingine kwa kiwango cha lami na mengine ni madaraja ya kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na maelezo mengine ya ziada yatatolewa kwenye bajeti yetu ambayo inatarajiwa kusomwa Jumatatu ijayo tarehe 17 na tarehe 18. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Stalike – Kibaoni yenye urefu wa kilometa 71 ni ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe

Magufuli na tayari barabara hiyo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu.

Swali langu kwa Serikali: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami katika barabara hii, ukizingatia Mkoa wa Katavi ni moja kati ya mikoa michache sana ambayo bado haijafanikiwa kuunganishwa Mkoa na Mkoa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu na Mkoa wa Katavi upo kwenye mchakato wa kupata barabara za lami. Kama nilivyosema, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, bajeti yetu inaanza kujadiliwa tarehe 17 na tarehe 18 hapa Bungeni. Nitapata fursa ya kuwatajia barabara ambazo tumetangaza kwa mwaka huu na mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie katika barabara muhimu ambazo zinajengwa kwa kiwango cha lami ni pamoja na kuunganisha Mkoa wa Katavi na maeneo mengine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Marais wetu waliopita akiwemo Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli waliahidi ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mbalizi – Shigamba:-

Je, ni lini sasa hiyo barabara itajengwa kwa kiwango cha lami? Nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ahadi zote za Viongozi Wakuu wa Nchi akiwemo Dkt. Hayati Magufuli, Mama Samia, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wengine, ahadi hizi lazima zitekelezwe kwa sababu ni ahadi ya Serikali na Serikali ipo kazini inafanya kazi na kazi inaendelea.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwaa Mbunge kwamba, barabara yake hii kama ilivyoahidiwa itafanyiwa kazi, itajengwa kwa kiwango cha lami, tupeani ushirikiano na muda si mrefu ahadi hiyo ya viongozi itatimia kabla ya 2025. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Umuhimu wa barabara ya Mkundi ni sawasawa na barabara ya Mugala kwenda Busambala. Je, ni lini Serikali itafikiria kujenga barabara hii katika kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara, mdogo wangu Mheshimiwa Kajeje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza eneo hili nalifahamu, mimi natoka katika Mkoa wa Mara na tumeshapata taarifa, Mheshimiwa Mbunge hapa ameulizia ili wananchi wasikie kama analisemea katika Bunge hili Tukufu. Mheshimiwa Mbunge tuliwahi kuzungumza nje ya *box*, inafanyiwa kazi na asubiri tarehe 17 na 18 atapata majibu sahihi. Kwa hiyo, watu wa Mwibara na Mkoa wa Mara kwa

ujumla na mikoa mingine yote tutazifanyia kazi. Ahsante.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 238

### **Mpango wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege - Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, mpango wa Serikali wa ujenzi wa uwanja wa ndege eneo la Kisumba, Wilayani Kalambo umefikia hatua gani kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa imejikita katika kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga kilichopo Mkoani Rukwa ambacho ni miongoni mwa Viwanja vya Ndege vinne (4) vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kupata ufadhili kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank - EIB*). Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za kupata Mkandarasi na kupewa Idhini (*No Objection*) kutoka *EIB*, kinachosubiriwa ni kupata fedha baada ya taratibu za kimkataba kukamilika.  
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege kwamba, baada



ya Serikali kukamilisha Ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya mikoa vilivyosalia ikiwemo Sumbawanga, Serikali itaendelea na ujenzi wa viwanja vidogo vya ndege kwa hadhi ya *airstrip* ikiwa ni pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashauri wananchi wa Kalambo kutumia Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga mara ujenzi wake utakapokamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHATS S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu ya Serikali naomba niulize maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; hii hadithi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege Sumbawanga ni hadithi ya muda mrefu na wananchi wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu. Sasa naomba kupata majibu ya Serikali ni nini ambacho kinakwamisha upatikanaji wa fedha kwa sababu tumekuwa tukisubiri muda mrefu ili ujenzi huu uanze mara moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sababu ujenzi wa uwanja ulioko Sumbawanga uko katikati ya Mji na kwa kuliona hilo Serikali iliamua kwa makusudi mazima kutenga eneo lingine na si kama *airstrip* kama ambavyo Naibu Waziri amejibu. Aliyekuwa Makamu wa Rais Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Dkt. Ghalib Bilal alifika eneo la Kalambo na kuweka jjiwe la msingi ili eneo lile liendeleo kulindwa. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba eneo lile halivamiwi ili itakapofika wakati wa kujenga uwanja mkubwa kusiwe na haja ya fidia? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotoa maelezo yangu kwenye jibu la msingi ni kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na Mheshimiwa Kandege anafahamu taratibu za Serikali, kama jambo ni makubaliano ya kimkataba lazima yakamilike. Hata hivyo, nipokee hoja yake kama kweli kuna ucheleweshaji tutalifanyia kazi ili uwanja huu ukamilike kama ambavyo tumeahidi kwenye jibu letu hapa kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipokee ushauri wake wa pili kwamba eneo hili ni kweli kwamba juzi nilikuwa Mtwara, hoja mojawapo iliyopo kule ni kwamba wananchi wamesogea karibu na eneo na wahitaji kulipwa fidia ambayo ni gharama nyingine kubwa tena kwa Serikali. Eneo hili litasimamiwa, lipimwe liwekwe mipaka na vizuizi ili libaki kwa matumizi ambayo limekusudiwa na wananchi wasianze kugombana na Serikali kwa kudai fidia ambayo itaongeza gharama pia katika maeneo hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake.

Na. 239

### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu Vijiji vya Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano ya simu kwenye Vijiji vya Igalula ambavyo havina mawasiliano ya simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ina jukumu la kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini ambayo hayana mvuto wa kibiashara. Mpaka sasa Mfuko wa Mawasiliano umeshatekeleza miradi 686 na bado kuna miradi katika kata 371 ikiwa inaendelea na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Igalula lina kata 11 ambapo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imetekeleza miradi sita ya mawasiliano katika Jimbo la Igalula ambapo imejengwa minara sita ambayo imetolewa na watoa huduma katika Kata tano ambazo ni Kizengi, Loya ambayo ina Miradi miwili, Lutende, Miswaki pamoja na Tura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata zenye watoa huduma wa mawasiliano katika Jimbo la Igalula ni 10 ambazo ni Igalula yenyewe, Kigwa, Loya, Lutende, Miswaki, Kizengi, Miyenze, Tura, Goweko pamoja na Nsololo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali, Kata ya Mmale na baadhi ya maeneo ya Jimbo la Igalula bado yana changamoto ya mawasiliano na kupitia Mfuko wetu wa Mawasiliano tunaendelea kufanya tathmini, ili tujiridhishe *specifically* kwamba kuna changamoto katika maeneo yapi ili yaingizwe katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zitakazotangazwa katika siku za usoni kadri upatikanaji wa fedha utakapokuwa unaruhusu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daud Protas Venant, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu

Waziri naomba nitoe taarifa, katika Jimbo la Igalula kuna watoa huduma wamekwishafika baadhi ya maeneo ambayo wamekwishasainiana mikataba ikiwemo Maguliathi, Migongwa, Makoyesengi na Mbulumbu lakini wameondoka mpaka sasa hivi hawajui nini hatima ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niulize maswali mawili ya nyongeza, Jimbo la Igalula ni miongoni mwa majimbo yenye changamoto kubwa ya mawasiliano na vijiji vingi vimekua, wananchi wana simu lakini hawana mawasiliano hasa katika Vijiji vya Songambebe, Kawekapina, Nyauwanga na Simbozamal. Sasa ni lini Serikali itaiwekea mpango wa kupelekea minara hasa vijiji hivi vilivyokuwa katika Jimbo la Igalula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; tuna huduma ya mawasiliano katika kata alizozitoa katika jibu la msingi lakini, huduma hizi zimekuja miaka mingi iliyopita, sasa mitandao imekuwa ikisumbua na wananchi hawapati huduma. Je, ni lini Serikali itakwenda kwa watoa huduma kukagua kwa sababu idadi ya watu imekuwa kubwa, wananchi kifika jioni haipatikani simu na huduma haipatikani. Serikali ina kauli gani kwa watoa huduma ili waweze kwenda kuipitia minara hii ili iweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Protas Daudi, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ameongelea kuhusu watoa huduma ambao wamefika na kuanza kufanya utafiti ili waweze kuweka minara. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi ambayo anaifanya kwa niaba ya wananchi wake wa Jimbo la Igalula. Mheshimiwa Mbunge alishafika katika ofisi zetu na

akatuomba tuweze kuhakikisha kwamba mawasiliano katika Jimbo lake yanapatikana na ndio maana mpaka sasa amesema kwamba, kuna watoa huduma tayari wameshafika katika eneo lake. Hii ni kwa sababu, Serikali imeenda kutekeleza ombi la Mheshimiwa Mbunge. Pia tufahamu kwamba, mikataba tunayowapatia watoa huduma ni mikataba ambayo inachukua takribani miezi tisa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama ambavyo amesema hatua ya kwanza watoa huduma wanayoifanya, ni kwenda kupata ile *lease agreement* pale ambapo mnara unatakiwa kwenda kujengwa. Hatua ya pili mtoa huduma anatakiwa kwenda kutafuta *aviation permit* ili aweze kuruhusiwa kujenga mnara. Hatua ya tatu ni kwenda kutafuta *environmental impact assessment permit* ili aweze kuruhusiwa na ndugu zetu wa mazingira. Baada ya hapo ndipo sasa apate *building permit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *process* zote ni *sequential process* ambazo hatua moja ikitokea ndio inatoa nafasi ya hatua ya pili kufanyika. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge baada ya kukamilika kwa huu mchakato mzima wa kupata hivi vibali, basi utekelezaji wa ujenzi wa minara hii katika Jimbo lake utatekelezwa bila kuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la pili ambalo ameongelea kwamba, kuna minara ambayo ipo lakini haitoi huduma stahiki. Ni kweli kabisa tunatambua kwamba kuna minara mingine ambayo ilijengwa miaka ya nyuma ambapo *population* ya eneo husika ilikuwa kidogo, iliweza kuhudumia wananchi waliokuwepo kwa kipindi hicho, lakini kwa sababu wananchi wanaendelea kuongezeka maana yake sasa minara hii inaanza kuzidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tumeshaelekeza watoa huduma wetu waende kufanya tathmini, ili wajiridhishe tatizo halisi ni lipi, kwa sababu kuna matatizo mengine ambayo yatahitaji kufanya *treating* tu ya

*antenna*. Mengine itabidi kuongeza *capacity*, tatizo lingine itabidi kuongeza nguvu ya *transmitter* na tatizo lingine ambalo litatufanya tukaongeze *antenna* zingine ili ziweze kuhudumia wananchi wa eneo husika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni lazima tathmini ifanyike kwa kina na kuna mengine ambayo yana *budget implication*, lakini kuna mengine ambayo ni matatizo ya kiufundi peke yake, tayari watoa huduma tumeshawaelekeza na tayari wameshaanza kufanya tathmini katika maeneo yote nchini ili kujiridhisha kwamba tatizo linalolalamikiwa linahusiana na nini hasa. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Eric Shigongo, swali kwa kifupi.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Matatizo yanayowapata wananchi wa Igunga ni sawasawa kabisa na matatizo yanayowapata wananchi wa Jimbo la Buchosa hasa katika Visiwa vya Kome na Maisome. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba ni lini watajenga minara katika maeneo hayo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Buchosa yameshaingizwa tayari kwenye mpango wa utekelezaji katika zabuni itakayotangazwa ya awamu ya sita ili eneo hilo sasa lipate mawasiliano kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Buchosa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa mujibu wa taarifa ya *TCRA* asilimia 68 ya Watanzania wako kwenye maeneo yenye mtandao wa kuweza kutoa huduma ya *internet*, lakini ni asilimia 26 tu wenye simu janja ama vifaa vingine vyovyote vinavyoweza kuwapa *access* ya *internet*. Sasa na changamoto kubwa ni kwa sababu ya kodi na vitu vinavyofanania hivyo, sasa kwa kuzingatia kwamba Wizara inataka kulfanya Tanzania iwe katika utaratibu wa kidijitali, wana mkakati gani basi wa kuhakikisha huduma hizi zinapatikana kwa gharama nafuu, ili Watanzania wengi waweze na kuwa na hivi vifaa na hatimaye kuweza kushiriki katika dunia ya TEHAMA na kidijitali? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyosema tuna changamoto hiyo kwa sasa, lakini sasa Serikali tunafahamu kwamba tunaenda kwenye uchumi wa kidijitali, lakini tunapoenda kwenye mfumo wa kidijitali maana yake ni kwamba tunahitaji kuwa na *internet penetration* na mpaka 2025 tufikie tuwe tumeshafikia asilimia 80 kutoka asilimia 43 ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya dijitali yoyote yanaendana na vifaa ambavyo *vita-support* matumizi halisi ya teknolojia husika. Mheshimiwa Mbunge pia anafahamu kwamba, tuko kwenye mchakato wa kuangalia namna bora ambayo itasababisha vifaa hivi vitakapokuwa vinaingia nchini, basi viwe vina bei ambazo zitawavutia Watanzania wengi kununua hizi simu ili waweze kutumia teknolojia ambayo itakuwa inatumika. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, sasa aulize swali lake.

Na. 240

**Kufuta Hati za Shamba la Kwamtii – Mkinga**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafuta hati ya mashamba yaliyotelekezwa kwa zaidi ya miaka 20 Wilayani Mkinga hususan shamba la Kwamtii ili ardhi hiyo igawiwe kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (Sura 113), kila mmiliki wa ardhi anapaswa kuendeleza ardhi yake aliyomilikishwa kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki. Kwa wamiliki wanaobainika kukiuka masharti ya umiliki, sheria hiyo imeelekeza hatua mbalimbali za kuchukua ikiwemo kubatilisha milki husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa mashamba yenye milki za hati Na. 14501 (Ekari 2,841) na hati Na. 4722 (Ekari 58) Kwamtii, Wilayani Mkinga yanayomilikiwa na Kampuni ya Kwamtii *Estate Limited* kwa matumizi ya kilimo yana ukiukwaji wa masharti ya umiliki ikiwemo wamiliki kushindwa kuyaendeleza na kukwepa kulipa kodi ya ardhi kikamilifu. Hata hivyo, imebainika kuwa, katika Daftari la Kumbukumbu la Msajili wa Hati, hatimilki za mashamba hayo zimewekwa rehani kwa kukopeshwa fedha na hivyo kuwa na *third part interest* (maslahi ya mtu wa tatu).



Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeelekeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kuanza kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutuma Ilani ya Ubatilisho kwa wamiliki. Hatua hiyo ikifanyika sambamba na kuwasiliana na Benki iliyotoa mkopo kama dhamana kuwataarifu wahusika kutafuta dhamana nyingine kutokana na masharti ya mashamba hayo kukiukwa. Mara baada ya milki za mashamba hayo kubatilishwa, hatua za kuyapanga, kuyapima na kuyagawa upya kulingana na mahitaji halisi sasa zitaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naishukuru Wizara kwa majibu haya. Swali la kwanza; kwa kuwa taratibu hizi za Ilani zimekwisha kukamilika na kwamba mmiliki huyu anatumia ardhi isivyo stahili. Je. Waziri anatuambia nini kwa kuwa taratibu hizi zimekamilika ni lini sasa hati ya mashamba haya zitafutwa baada ya kupelekwa kwa mamlaka ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa barua ya mapendekezo ya kufuta hati ya shamba hili yalizingumzia vile vile Shamba la Mwele ambalo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kutembelea Mkinga alitoa maagizo kwamba, ardhi ile imegwe kutoka kwenye shamba la Serikali kwa sababu, limetelekezwa kwa zaidi ya miaka 20. Je. Waziri yupo tayari kufuatilia jambo hili ndani ya Serikali ili agizo lile la Waziri Mkuu liweze kufanyiwa kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza amezungumzia kwamba taratibu zile zinazotakiwa kufuatwa katika ubatilishwaji zilishakamilika. Naomba kukiri ni kweli kwasababu barua ya ubatilisho ilitoka tarehe 10 Machi, 2020

maana yake kufikia Juni, 2020 tayari utaratibu ule ulikuwa umekwisha. Lakini wakati huo huo mmiliki huyu alileta utetezi wake akitetea kwamba asiweze kunyang'anywa kwasababu alizokuwa amezilieleza. Lakini baada ya kuangalia pia ilionekana kwamba miliki ile ilikuwa imewekezwa kama dhamana kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini hiyo pia haituzuii kama wizara tumetoa maelekezo kwenye halmashauri kwasababu ile hati imeshawekwa dhamana katika Benki, na Benki yenyewe ni Benki ya Nje kwa hiyo tumeshaelekeza na tayari wamekwisha toa ilani kwa ajili ya kubatilisha tena wamempelekea na yule mmiliki wa Benki ili ajue kwamba dhamana aliyonayo kisheria kwa sheria za Tanzania sasa haitakiwi iwe kule kama ambavyo inapaswa.

Kwa hiyo, tunasubiri hizi siku zikiisha basi tutaweza kufanya kile ambacho kinatakiwa kufanywa kisheria na watu wa Halmashauri ya Mkinga wataweza kufaidika na lile shamba. Namuomba tu Mheshimiwa Mbunge basi awe na subira katika hilo kwasababu tayari taratibu zinafanyika na ilani imekwishatumwa kwenye ile Benki ya Nje pamoja na kwa mmiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali lake la pili anaongelea suala Mweru ambalo lilikuwa na maelekezo pia ya Waziri Mkuu. Kwanza nichukue fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dunstan Kitandula kwasababu amekuwa akifuatilia sana. Nakumbuka hata mwaka jana, mwaka juzi kuna shamba la *MOA* alilipigia kelele taratibu zilifuatwa likabatilishwa na wakaweza kupewa na sasa wananchi wanalitumia kwa mujibu wa waliyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili naomba nimuhakikishie kwamba, tutachukua *speed* isiyo ya kawaida tunahakikisha kwamba tunafanya ufuatiliaji na kama umemsikia pia Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita amesema hana mzaha na wale ambao wana hodhi ardhi bila ya kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Na sisi kwa kasi ile ile tutaendelea mbali na hilo shamba la Mweru tutaangalia pia na mashamba mengine katika maeneo mengine ambayo wameyahodhi ili tuweze kuchukua hatua stahiki na yaweze kutumika kwa matumizi ambayo yataleta faida kwa wananchi lakini kwa Taifa kwa ujumla. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkansi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 241

### **Changamoto ya Maji - Nkasi Kaskazini**

**MHE. AIDA J. KHENANI** atauliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza changamoto ya maji katika Wilaya ya Nkasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika; hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Nkasi ni wastani wa asilimia 48. Katika kutatua changamoto ya huduma ya maji, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wilaya ya Nkasi imeendelea na ujenzi wa jumla ya miradi 12 ambayo ni Kirando, Kabwe, Kisula, Isale, Mpasu, Matala, Kantawa, Sintali, Chonga, Kate, Mtambila na Katongolo ambapo itakamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mradi wa uchimbaji wa visima virefu sita umekamilika katika vijiji vya Ntumbila,

Kachehe, Itindi, Lyazumbi, Nkomo II na Milundikwa. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji utafanyika katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo utahusisha matanki matatu ya maji yenye ukubwa wa lita 90,000 na lita 45,000 na vituo vya kuchotea maji 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mji wa Namanyere, Serikali inaendelea na uboreshaji wa huduma ya maji kwa kutumia chanzo cha maji cha bwawa la Mfili ambapo kazi mbalimbali zitafanyika ikiwemo ufungaji wa pampu mbili katika bwawa la Mfili, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 3.9, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa tanki la lita 500,000 la kuhifadhi maji. Kazi hizo mradi zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nimeyasikia majibu ya wizara. Kwa kuwa mpango wa Serikali ulijiwekea malengo kufikia mwaka 2025 upatikanaji wa maji vijijini itakuwa ni asilimia 85. Na leo ni mwaka 2021 na umekiri hapa kupitia majibu yako takwimu ambazo umezisoma kwamba upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Nkansi ni asilimia 48 tu. Kwanza takwimu hizi si halisia. Lakini napenda kuwaambia Serikali kwa kuwa mpaka sasa tuna asilimia 48 hamuoni sasa kuna jitihada za ziada za kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika ili kuweza kufikia asilimia 85 kama malengo tuliyojiwekea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali la Pili, huu mradi wa maji Namanyere wananchi wameanza kuangalia mabomba toka mwaka jana hawapati maji mpaka leo. Ningependa kujua kuna mkakati upi wa ziada wa Serikali wa kuweza kupelekea wananchi wa Namanyere na Kata zote za Jimbo la Nkasi Kaskazini maji ili waendane na kauli mbiu ya Mama Samia ya kumtua mama ndoo kichwani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mpango wa Serikali kufika mwaka 2025 kadri ya ilani ya Chama Tawala inavyotaka vijijini maji yatapatikana kwa asilimia 85 na zaidi ikiwezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nipende kukutoa hofu Mheshimiwa Mbunge na nikupongeze unafuatilia kwa makini sana masuala haya ya wananchi wako na wewe ni mwanamke ndio maana unaongea kwa uchungu kwasababu unafahamu fika kubeba maji kichwani kwa umbali mrefu namna ambavyo ilivyotabu.

Kwa hiyo tutahakikisha tunawatua kina mama ndoo kichwani. Wewe ni Mbunge mahiri mwanamke na mimi ni Naibu Waziri Mwanamke wote tunafahamu adha ya kubeba maji kichwani tutashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tunafahamu fika RUWASA haikuwepo na kwa mwaka mmoja tu tumeona namna ambavyo RUWASA imefanya kazi kwa bidii. Na kufufua miradi ambayo ikisuasua na sasa hivi maji yanapatikana mabombani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Ziwa Tanganyika Mheshimiwa Aida, kama ambavyo tumetoka kuongea kwa kirefu hapa majuzi wakati tunapitisha bajeti yetu. Huu ni mpango mkakati wa kutumia vyanzo hivi vya uhakika, kwa hiyo Ziwa Tanganyika nalo lipo kwenye mikakati ya wizara tutahakikisha tunalitumia ili kuona kwamba mabomba yapate kutoa maji na sio kushika kutu. Kwa hiyo, haya yote uliyoyaongea yapo kwenye utekelezaji wa wizara na ifikapo mwaka 2021/2022 mwaka mpya wa fedha Ziwa Tanganyika nalo tayari lipo kwene mpango mkakati wa utekelezaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumalizie swali la mwisho Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 242

**Ukosefu wa Maji - Jimbo la Newala Vijijini**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaimarisha na kuboresha miundombinu ya maji ya Mamlaka ya Maji Makonde ili Wananchi waweze kupata maji ya uhakika?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kuboresha upatikanaji wa maji Newala Vijijini ambapo kwa sasa uzalishaji ni ujazo wa lita 6,700 tu kwa siku badala ya lita 23,741?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya maji ya Mamlaka ya Maji Makonde inayohudumiwa Wilaya za Newala, Tandahimba na Nanyamba.

Katika kutatua changamoto hiyo, Serikali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ambapo katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 kazi zinazofanyika ni kukarabati mitambo na mfumo wa umeme katika vituo vya kuzalishia na kusukuma maji. Utekelezaji wa kazi hizi unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka meta za ujazo 6,700 kwa siku hadi meta za ujazo 11,116 kwa siku, kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata suluhisho la kudumu la tatizo la maji katika maeneo hayo, Serikali kuanzia

mwaka 2021/2022 imepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuongeza idadi ya visima vya kuzalisha maji kutoka 6 hadi 12 kwenye Bonde la Mitema pamoja na kupanua miundombinu ya kusafirisha maji uchimbaji wa visima utaongeza uzalishaji wa maji kutoka meta za ujazo 11,116 hadi Meta za ujazo 23,741 kwa siku. Kukamilika kwa kazi hizo kutaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 58 za sasa hadi asilimia 95.

Vilevile Wizara ya maji kupitia *RUWASA* katika mwaka wa fedha 2020/2021, imeendelea na utekelezaji wa miradi ya maji Mchemo na Chiule iliyotarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021 na miradi ya maji Mtongwele, Miyuyu na Mnima inayotarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Katika mwaka 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 1.95 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali katika Wilaya Newala Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mpango wa muda mrefu, Serikali ilipata mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* India jumla ya dola za Marekani Milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa Miji 28 ukiwemo mradi wa Makonde; ambapo maeneo yatakayonufaika ni vijiji 155 vya Wilaya ya Newala. Ujenzi unatarajiwa kuanza wakati wowote katika mwaka wa fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante. Naomba kuiuliza wizara maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatizo la maji kwenye Jimbo la Newala Vijijini limekuwa ni sugu, wananchi wa Newala Vijijini wanakunywa maji ya kuokota ambayo wanaokota kipindi cha mvua, maji ambayo huwa yanaoza na yanatoa harufu. Lakini tunacho chanzo kikubwa cha Bonde la Mitema ambalo Serikali ikiwekeza kwa kiasi kikubwa bonde lile litatua kabisa changamoto za maji kwa sababu maji yaliyopo katika

bonde lile yana mita za ujazo zipatazo 31,200 lakini mahitaji ya wananchi wa Newala, Tandahimba pamoja na Nanyamba kwa siku ni mita za ujazo 23,441.

Je Serikali imejipangaje kuhakikisha inaweka fedha za kutosha katika bonde la Mitema ili tatizo la maji liweze kukoma na wananchi waweze kupata maji ya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika kituo cha Mto Ngwele kulikuwa na tatizo la *pump house* pamoja na *transformer*. Lakini bahati nzuri Januari mwaka huu *pump house* imerekebisha na TANESCO wameshapelekwa pale *transformer* iko pale haijafungwa hadi leo hii ikaweza kusukuma maji. Nini kauli ya Serikali kwasababu wananchi wanaendelea kutaabika kupata maji wakati *transformer* iko pale wanashindwa kuifunga. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge kwanza nakupongeza sana wewe ni Mbunge wa Jimbo, mwana mama Hodari na umekuwa ukifuatilia kwa uchungu sana masuala la maji ili kuokoa kina mama wenzako kuhakikisha wanatuliwa ndoo kichwani kama ambavyo wizara tunakesha, tunafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba kina mama lazima tuwatue ndoo kichwani na maji yapatikane umbali mfupi kutoka kwenye makazi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake namba moja anauliza fedha za kutosha kuwezesha bonde la Mitema. Hii ni moja ya kazi ambazo tumeagiza *RUWASA* waweze kushughulikia, hii itafanyika ndani ya mwaka wa fedha ujao na kuona kwamba tuanze kuuona usanifu unakamilika na kila kitu kinakwenda vizuri ili maji yaweze kupatikana kwenye chanzo cha uhakika. Wakati tuna hitimisha bajeti yetu nimeongelea suala la Newala hata mimi ni mwana mama nisingependa kuona watu wanaendelea kutumia maji ya kuokota kwa karne hii na tumshukuru Mungu tumempata Rais



mwana mama ambaye kiu yake kubwa ni kuona kina mama wanatuliwa ndoo kichwani. Mheshimiwa Mbunge Maimuna hili tutashirikiana kwa pamaja kuona kwamba tunakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusiana na *transformer* ambayo ipo pale. Sisi kwa upande wa wizara yetu tuliweza kushughulika na *pump house* na imeshakamilika. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Nishati kuona kwamba sasa ile *transformer* inakwenda kufungwa haraka iwezekanavyo ili matumizi ya umeme kwenye kusukuma maji yakaweze kufanyika na watu wakanufaike na mradi ambao umeshakamilika.

**MHE COSATO D. CHUMI:** Hoja ya kuahirisha mjadala.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele. Kwanza ni wageni tulionao asubuhi hii hapa Bungeni.

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma wanaotokea Jijini Mwanza wakiongozwa na Ndugu Devotha Daniel. Karibuni sana (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambaye ni shemeji yake kutoka Mamlaka ya Maji Mafinga, Mkoa wa Iringa Ndugu Joyce Malongo. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 23 wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma ambao ni wenyeji wa Ukerewe Mkoani Mwanza wakiongozwa na Ndugu Musa James. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa David Kihenzile ambao ni umoja wa Wanavyuo wanaotoka Wilayani Mufindi yaani Mufindi *Intellectual Communty* walioko Mkoani

Dodoma wakiongozwa na mwenyekiti Ndugu Jofrey Mtasiwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Kasalali Mageni ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Sumve wakiongozwa na Ndugu Walwa Shikome. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 5 wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Buchosa waliopo Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Evalist Masumbuko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambaye ni Mbunifu wa Mavazi kutoka Mkaoni Mbeya, Ndugu Deborah Mwankenja. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambaye ni Mpiga Kura wake kutoka Arumeru Mashariki Jijini Arusha na huyu ni Ndugu Edga Manyara. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao siku ya leo hapa Bungeni lakini lipo pia tangazo linalotoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba siku ya Jumatatu tarehe 17 Mei, 2021, saa saba kamili Mchana mara baada ya kusitishwa Kikao cha Bunge kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wote kuhusu huduma ya vifurushi yaani *bundle services* vinavyotolewa na Makampuni ya Simu. Mafunzo hayo yatatolewa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na yatafanyika katika ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria mafunzo hayo muhimu ili mkishafahamu ninyi basi inakuwa rahisi kuzungumza na Wapiga Kura wenu na kuwaelimisha.

Baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya dharula.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Hoja ya kuahirisha mjadala.

**NAIBU SPIKA:** Hoja ya kuahirisha mjadala Kanuni gani.

### HOJA YA KUAHIRISHA MJADALA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 79(i) ambacho kinasema Mbunge anayependa mjadala unaondelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye anaweza kutoa hoja kwamba Mjadala sasa uahirishwe na atataja mdajala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

**NAIBU SPIKA:** Haya, nimekupa fursa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na kuomba kwamba mjadala uahirishwe kwa sababu kwa siku kama ya tano au sita sasa pale bandarini ambapo ndiyo chanzo cha mapato mengi ya Taifa letu katika kuendesha miradi mbalimbali na kufanikisha miradi ambayo tunajadili hapa katika bajeti, malori hayashushi wala kupakia mizigo. Maana yake ni kwamba uchumi kwa namna fulani umesimama wakati tunazungumzia ushindani kati ya bandari yetu na bandari za majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii hatuwezi kukaa kimya na kuacha mambo ya namna hii yaendele. Ndiyo maana najenga hoja tuahirishe mjadala ili tujadili jambo hili nyeti ambalo kwa namna moja au nyingine linaenda kuathiri uchumi wa Taifa letu. Kuna mizigo pale ya kwenda kwenye mradi wa Mwalimu Nyerere, *SGR* na kwenda nchi jirani ukizingatia nchi yetu ni *transit*, imekwama pale na wakati huo huo tunatarajia kwamba bandari yetu iwe na ushindani dhidi ya bandari nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii, ndiyo maana naomba tuahirishe mjadala tujadili jambo hili ambalo ni nyeti katika Taifa na hivyo naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, naona hoja imeungwa mkono lakini, wacha tuiweke vizuri kwanza kabla ya hatua hiyo. Kanuni inataka useme uahirishwe hadi wakati gani ili mimi sasa niweke vizuri hilo nijue hapa nittoa muda gani.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mjadala uahirishwe kwa muda wa saa moja, hili ni jambo nyeti sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hiyo ndiyo hoja yake. Mimi nataka kuiweka vizuri kwa sabbau Kanuni inanataka niweke vizuri kabla ya ninyi kuhojiwa na kufanya maamuzi juu ya jambo hili.

Kwa uendeshaji mzuri wa Bunge, hatutaweza kuahirisha Bunge kwa saa moja, tutaweza kuahirisha Bunge kwa dakika 20 ili tupate fursa ya kupata taarifa mahsusi kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Sasa wale mliotaka kuunga mkono hoja hii, sasa mnaweza kumuunga mkono Mheshimiwa aliyetoa hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu hoja imeungwa mkono.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Ni hoja hii au nyingine?

**MBUNGE FULANI:** Nyingine

**NAIBU SPIKA:** Na wewe unataka tuahirishe Bunge?

**MBUNGE FULANI:** Kwa muda kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Basi wacha tumalize hoja hii kwanza.  
(Kicheko)

Kwa hiyo, tutazungumza kuhusu hoja hii kwa dakika 20. Upande wa Serikali nadhani Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi wako hapa lakini tutawaona watakaosimama ili wazungumzie hoja hii.

Hoja hii itachangiwa kwa muda mfupi kwa sababu nimetoa dakika 20. Sasa Wabunge wanaotaka kuchangia wasimame. Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Ruhoro, Serikali nimewaona wawili, Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Mwakagenda, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Kunambi, Mheshimiwa Nyongo na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Kakoso.

Nadhani hawa wanatosha na kwa idadi iliyoko hapa ni kama itakuwa dakika moja moja, nitatoa dakika mbili kwa kila Mbunge. Tutaanza na Mheshimiwa Mwijage. Upande wa Serikali, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi mjiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Chumi. Huduma za Bandari ya Dar es Salaam zinasikitisha hususan katika kipindi hiki ambako Wabunge tumeacha shughuli zetu majimboni tumekuja hapa kupanga maendeleo ya Watanzania kwa mwaka mmoja au miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ndiyo ng'ombe wa maziwa ya nchi hii. Kuna nchi jirani Rais wake aliwahi kututania au kutukebehi kwamba yeye alikuwa tayari aje apewe Uwaziri wa Bandari aweze kuunganisha nchi yake na ya kwetu kwa sababu ya uchumi wa nchi hii. Kama bandari yetu ingeweza kutumika vizuri kuna kipato kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba uingiaji na utoaji wa mizigo bandarini unapelekea magari

yetu kukaa pale kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nchi nyingine na ndiyo maana Bandari ya Beira ikazaliwa, Bandari ya Beira pamoja na *disadvantage* nyingi za Beira, magari mengi yalihama kwenda Beira, Zambia kwa sababu ya utendaji wetu mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wabunge lazima tuisaidie Serikali kwa kuwaelewesha na Serikali lazima wawe tayari kujifunza kutoka kwetu na kwa wataalam wa sekta hiyo kwa maana ya *transporters* na wadau wote namna gani tunaweza kuitumia bandari yetu kama alivyosema Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwamba bandari lazima itumike ipasavyo. Mtu mmoja alisema hoja sio *location advantage* bali ni kutumia *location advantage*. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimeshtuka sana niliposikia kwamba Bandari ya Dar es Salaam inafanya kazi kwa kusuasua. Uchumi wetu sisi kwenye Jimbo la Ngara tunategemea sana Bandari ya Dar es Salaam ambapo magari makubwa yanayotokea pale bandarini yanapita kuelekea Rwanda na mengine yanapita Ngara kuelekea Burundi. Kwenye miji yetu ya Kabanga, Benako na Rusumo tunategemea sana haya magari yatoke bandarini, yaje mpaka pale, yapaki, wale madereva waweze kulala kwenye hoteli zetu na kununua vyakula na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha magari haya kuchelewa kutoka bandarini kinaathiri uchumi wa wananchi wa Jimbo la Ngara. Ndiyo maana nimesimama kuunga mkono hoja hii na kuiomba Serikali iweze kufanya haraka sana kushughulikia changamoto iliyoko bandarini ili wananchi wangu wa Jimbo la Ngara wasipatwe na madhara ya kukosa kuuza bidhaa zao kutokana na magari kuchelewa kutoka bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba tutambue kwamba bandari hii imetoa ajira kubwa sana kwa madereva na vijana wetu wa Kitanzania. Hivyo, kitendo cha bandari kutofanya kazi kwa siku zaidi ya mbili au tatu kinaathiri uchumi si tu wa Taifa bali ni pamoja na ajira za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye hoja kama hizi kengele ikishagonga unakaa zako mwenyewe.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mimi nataka tu kusema kwamba tumewekeza fedha nyingi sana katika kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Kuanzia gati namba 1 mpaka 10 zinajengwa kwa fedha nyingi na bahati nzuri sisi wengine ni Kamati ya miundombinu tumeshuhudia. Leo hii ikiwa kunaonekana kuna tatizo la kushusha mizigo au kupakia kuitoa pale inaathiri sana uchumi wetu lakini pia fedha tulizowekeza hazirudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri basi Serikali ikatuambia ni juhudi gani zinafanyika kuhakikisha inaondoa changamoto hii. Kwa sababu leo tuko kwenye ushindani na bandari zingine zinazotuzunguka lakini kijiografia Bandari yetu ya Dar es Salaam iko vizuri. Ni vizuri tukaboresha usimamizi wa bandari yetu ili kuendelea kukuza uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni masikitiko makubwa. Naiomba Serikali ichukue hatua stahiki ili kuweza kuokoa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naunga mkono hoja hii kwa sababu kubwa mbili. Ya kwanza, tunafahamu kabisa kwamba nchi yetu ya Tanzania imebahatika kuwa na bandari nzuri na nchi nyingi zinazotuzunguka hazina bandari, zinatutegemea sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipokuwa makini inawezekana kuna watu wanaweza kuja nchini kwetu wakatumia ujanja wa kuhujumu bandari yetu. Hivyo basi, tunaomba kujua kwa nini kiongozi wa bandari hajatoa taarifa kama kuna tatizo lolote kuhusiana na upakiaji na upakuaji pale bandarini? Naomba kama Bunge tusimame na kujua hakika kwa nini tunaenda kupoteza fedha zetu kwa siku mbili na nchi ikakaa kimya? Mimi ninasimamia sehemu hii kusema kwamba kuna haja ya kutuma watu wa intelijensia kujiridhisha kama hakuna hujuma inayopita ndani kuhakikisha kwamba bandari hii haifanyi kazi ili kuwapa kazi bandari zinazopingana na sisi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu kwamba katika nchi yetu hii tunao majirani zetu ambao wana bandari ambao sio bora kama Bandari ya Dar es Salaam. Hivyo basi, tunahitaji kuhakikisha tunailinda bandari yetu na kama kuna uzembe wa kiongozi yeyote katika bandari ile, Serikali ichukue hatua na sisi tusimamie tuhakikishe inasimama. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, unapotaka kutatua changamoto yoyote lazima utambue kwanza chanzo cha tatizo. Tukianza hapo tunaweza kupata suluhu njema kabisa.



Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahisema hapa siku moja, changamoto kubwa ya Taifa letu ni uzalendo, wengi hatuipendi nchi yetu. Nachelea kusema yamkini kukawa na *sabotage*. Laiti kama ingekuwa uwezo wangu binafsi, kama kuna mtu anakaimu hiyo ofisi ameanza kufeli leo maana nadhani Mkurugenzi Mkuu bado hajapatikana, yule mwingine amewekwa pembeni kidogo. Kama kuna anayekaimu, ameanza kufeli kuanzia sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taasisi yoyote ukiona hai-*perform* changamoto ni kiongozi mkuu wa taasisi. Ukiona taasisi ina rushwa iliyokithiri, chanzo sio *management*, ni mkuu wa taasisi. Kwenye taasisi kuna kitu kinaitwa *institutional behavior*, huu ni utamaduni au tabia ya taasisi katika mwenendo wa utekelezaji wa majukumu yake. Kwa hiyo, ukiona kuna changamoto ya namna hii, usipambane na hao wadogo wadogo, toa yule kichwa, mambo yatabadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kuna Waziri anayeshughulika na Wizara hii, Naibu Mawaziri wako hapa, kama Wabunge tungenda kusikia hatua walizochukua hadi sasa. Tunapoteza fedha nyingi na kimsingi tatizo hili linakwenda kumgusa kila Mtanzania. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Bandari ni kiungo muhimu sana kwa uchumi wa Taifa lolote lile. Zaidi ya asilimia 80 ya biashara zinafanyikia majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu wakati anakuja kuhutubia hapa alisema kabisa aatahakikisha anaongeza ushindani kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Sasa kwa haya yanayoendelea hamna mfanyabiashara yeyote au hamna nchi yoyote itakuja Tanzania kama kwa wiki nzima malori yako pale, kuna *damage cost*, gari ikikaa pale kwa muda mrefu ina maana wale madereva na lile lori linakuwa *charged*. Ndiyo maana pia, mzigo ukikaa sana pale bandarini bidhaa zinakuwa adimu hapa. Kama wiki tatu nyuma, *white cement*

hapa Dodoma ilipanda bei kutoka Sh.25,000 mpaka Sh.50,000 wakasema mzigo umekwama bandarini. Kwa hiyo, kuna athari kubwa sana kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama nchi lazima tuhakikishe mosi, magari hayakai sana bandarini yaani mzigo ukifika unapakuliwa na kuondoka. Vinginevyo, hizi nchi za Burundi, Uganda na Rwanda, wata-*shift*, kwenda Bandari ya Mombasa na hapa kwetu tutakosa hayo mapato. Kwa hiyo lazima tuelezwe ni nini kinasababisha kunakuwa na uzembe kwenye upakuaji wa mizigo inapofika bandarini. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *impact* ya kuchelewesha kupakia na kushusha mizigo ni kubwa kuliko tunavyoifikiria. Bandari ya Dar es Salaam *geographically* ina *advantage* kwa nchi zinazotuzunguka, nchi zaidi ya nane zinategemea Bandari ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma tulipambana, kulikuwa na kitu kinaitwa *single territory custom*, ilikuwa fedha za kodi za Congo tunazikusanyia Bandari ya Dar es Salaam, ilitukimbizia wateja wakaenda Beira. Kulikuwa kuna tatizo la ku-charge VAT kwenye *auxiliary services on transit goods*, lilikuwa linatufukuzia wateja wanakwenda Beira, tukalifuta. Leo linakuja suala la kupakia na kushusha. Tatizo sio hilo tu, hata ukienda kwenye *floor meter* na penyewe ni tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam ina uwezo wa kupakia na kushusha mizigo zaidi ya tani milioni 4 kila mwaka. Tunapitisha mzigo wa tani 5000,000 za...

## T A A R I F A

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ninayotaka kuitoa kwa mzungumzaji ni kwamba Bandari ya Dar es Salaam kwa mwaka inapitisha tani milioni 17 za mizigo. Hiyo ni Taarifa ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya pili jambo hili mimi ninavyolifahamu ni kwamba siku ya Ijumaa ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, sasa hiyo ni Taarifa au unataka kuchangia?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Ni Taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Taarifa mpe kwenye kile alichokuwa anazungumza yeje unamuongezea nini?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ninayoitoa amesema ni tani milioni nne, ni tani milioni 17 kwa mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nyongo unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. STANLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea na kumuongezea tu ni kwamba milioni 4 ni kwa *hard cargo* na kuna hiyo *amount* nyingine inayobaki kwa ajili ya *liquid cargo* kwa maana ya mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana kwenye *floor meter*, kuna wizi mkubwa unaendelea lakini bado kwenye kupakia na kushusha kuna hujuma inaendelea kwenye *fork lifts*. Sasa hivi kuna tatizo la *fork lifts* ambalo limesababisha kutokushusha na kupakiwa kwa mizigo. Watu wameomba hata walete *fork lifts* za binafsi lakini uongozi wa bandari umekataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya hapo nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Kakoso kwamba angechangia kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Miundombinu lakini nimeletewa taarifa hapa kwamba tayari Serikali ina majibu juu ya jambo hili kwa hiyo, tuwasikilize halafu nitatoa maelekezo baada yao. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kuonesha ni kwa kiasi gani wanajali maendeleo na uchumi kwa ujumla kwenye Taifa letu. Pia kila jambo ambalo linaweza kuwa na dalili ya kuleta taabu wako tayari kuishauri Serikali ni jambo gani lifanyiwe kazi kwa haraka ili kusindeele kuwa na mdororo wa namna yoyote katika utendaji kazi wa Serikali na ukuzaji wa uchumi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalifahamu jambo hili na imekwishaanza kulishughulikia. Naomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira kidogo kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanza safari asubuhi hii na atakuwa bandarini kuhakikisha kwamba yale yote yanayojiri pale Serikali inatekeleza wajibu wake na kuhakikisha matatizo yoyote yanachukuliwa hatua. Pia Serikali inahakikisha utaratibu mzima wa uendeshaji wa bandari unarudi katika utaratibu wa kawaida na matatizo yaliyojitokeza yaweze kuondolewa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge watupe nafasi hiyo na tumuache Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ameshakwenda huko kwa ajili ya jambo hilo, nadhani tutakapokuwa tumelikamilisha Wabunge wote wataona ni kwa kiasi gani Serikali imetekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika hali ya kawaida hoja ikishatolewa huwa inabidi ifungwe na mwenye hoja baada ya mchango halafu tufikie mahali, lakini kwa taarifa hii iliyotolewa na Serikali, nadhani tuwape hiyo leo kwa sababu ndiyo Waziri Mkuu ameenda huko kushughulikia jambo hili. Nafikiri mtoa hoja ataafiki maelezo hayo ya Serikali.

Kwa hiyo, nafikiri tutakaporejea Jumatatu pengine mambo yatakuwa yameshabadilika katika hizi siku mbili tatu hapa. Kama kutakuwa bado na changamoto mahali, basi tutalianzia hapo ambapo leo tumepewa taarifa hiyo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

### **UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, kwa kawaida Bunge letu huwa linaongozwa na Mheshimiwa Spika akisaidiwa na Naibu Spika, pia wanakuwepo Wenyeviti watatu kwa ajili ya kusaidia pale ambapo kazi za Bunge zinakuwa ni nyingi na pia kwa uendeshaji mzuri tu wa Bunge letu, kwa sababu lina vikao vingi, huwa kuna Wenyeviti watatu.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, kwanza wote tukae. Waheshimiwa Wabunge mliosimama mkae na ninawaomba Waheshimiwa mnaozungumza msikilize. Kama inavyoonekana kwenye Orodha ya Shughuli leo, kuna shughuli ya Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge. Kanuni ya 7 ya Kanuni za Bunge imeweka uwepo wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao humsaidia Mheshimiwa Spika kuongoza vikao kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa kanuni zetu.

Utaratibu wa kuwapata wagombea wa nafasi ya Wenyeviti wa Bunge umewekwa katika Kanuni ya 13. Mchakato husika unaanza kwa Kamati ya Uongozi

kupendekeza majina sita kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia jinsia, lakini pia pande zetu mbili za Muungano. Baada ya hapo majina hayo hupelekwa Bungeni ili Bunge lipigie kura majina matatu.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 13 na taratibu zetu, Jumatatu tarehe 10 Mei, 2021 Kamati ya Uongozi ilikutana na kwa kauli moja ilipendekeza majina matatu ya Wenyeviti wawili na Makamu Mwenyekiti mmoja ili yaweze kuwasilishwa Bungeni na Bunge liombwe kuyathibitisha. Majina ya Wabunge waliopendekezwa na Kamati ya Uongozi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama; tunaye pia Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria; na pia yupo Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, ambaye ni Mbunge wa Mufindi Kusini. Huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge letu lilikwishaweka utaratibu kwamba chaguzi zinazofanyika hapa Bungeni, iwapo idadi ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo na vigezo vinavyohitajika vimetimizwa, basi wagombea hao wanapita bila kupingwa. Utaratibu kama huu ulitumika kwenye Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge katika Bunge la Kumi na pia Bunge la Kumi na Moja ambapo Kamati ya Uongozi ilipendekeza majina matatu na baadaye majina hayo yalithibitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nafasi zilizopo za Wenyeviti wa Bunge ni tatu; na kwa kuwa Kamati ya Uongozi imependekeza majina matatu; Bunge hili katika kikao chake cha leo, siku ya Jumatano, tarehe 12 Mei, 2021 linaombwa kuwathibitisha Wabunge hao kuwa Wenyeviti wa Bunge, ili kupata uamuzi wa Bunge. Sasa kwa utaratibu wetu wa kawaida nitawahoji.

Waheshimiwa Wabunge, nawahoji kuhusu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Waheshimiwa Wabunge Waliotajwa hapo juu  
Walithibitishwa na Bunge kuwa Wenyeviti wa Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Bunge zima limeafiki. Bunge zima kwa kauli moja limeafiki hawa kuwa Wenyeviti wetu watatu. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuwapongeza sana viongozi wetu hawa, wanaongoza kamati zao vizuri na watatuongoza vizuri hapa Bungeni wakati watakapotakiwa kusimamia vikao.

Mheshimiwa Spika anawatakiya kila la heri katika kupokea majukumu hayo mazito ya kuongoza vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Wabunge hao watatu ambao tumewachagua kuwa sehemu ya uongozi wa Bunge hawajapata fursa ya kujieleza kwenu wala kusimama, nitawapa kila mmoja wao dakika moja ya shukrani.

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema. Nachukua nafasi hii kushukuru Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi; namshukuru Spika na Kamati ya Uongozi na kubwa, kuwashukuru Wabunge. Kazi hii ya Kiti anayoifanya Naibu na Mheshimiwa Spika siyo kazi ndogo, lakini inakuwa nyepesi ikipata ushirikiano kutoka kwenye *floor* au kwenye *panel*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba na niwahakikishie utumishi wangu kwenu utakuwa wa weledi

mkubwa na kuthamini michango yenu na kuwaheshimu nyie.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ulinipa nafasi ngoja nichomekee hapa hapa. Tatizo kubwa la bandari wame-*migrate* kutoka mfumo wa *TANCIS* wamekwenda kwenye mfumo wa *Electronic Single Window System*. Aliyefanya hivi amefanya *trial and error* ndio anasababisha Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa kila jambo, lakini pia nakishukuru chama change, uongozi wake pamoja na uongozi wa Bunge kwa kuniadini kipindi cha Bunge la Kumi na Moja; na leo kwa mara nyingine. Naahidi kuendeleza uadilifu na kufanya kazi kwa moyo mmoja kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana, asanteni. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii, lakini nikishukuru chama changu, Kamati Kuu na vikao vyote. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe pia kwa heshima kubwa hii. Naishukuru Kamati yangu pamoja na Wabunge wote kwa kutupitisha kwa nafasi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge mpya, ni fursa nzuri pia ya kujifunza katika uongozi na niwaahidi kwamba nitatoa ushirikiano mzuri na kuwa msaidizi wako



wewe na Mheshimiwa Spika kwa uaminifu na uadilifu wangu wote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mmewaona hao ndio Wenyeviti wetu.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona jicho lako lilinisahau. Niliomba idhini ya Kiti chako kwa jambo la dharura, ukasema umalize kwanza hoja ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Kwanza ngoja, ngoja tuweke vizuri. Siyo hoja ya kukusahau. Inabidi usimame hoja nyingine ikiwa imekwisha. Kwa hiyo, unasimama upya tu kama ulivyosimama sasa. Kwa hiyo, hoja ya kukusahau haipo. Sawa, sasa umepewa nafasi.

### HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ambayo inasema; “Baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi na la dharura na muhimu kwa Umma.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwako; tunaona Serikali kwa nia njema imetangaza ajira kwa kada ya afya 2,726 na kwa kada ya ualimu 6,949. Wakati tunachangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani tulionesha umuhimu na tatizo la watu kukosa namba za *NIDA* na vitambulisho vya *NIDA* katika maeneo mengi, hasa Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine ambayo iko pembezoni na nchi nyingine na mikoa mingine ambayo iko katikati ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa mahususi katika tangazo la ajira hiyo ni kuwa na namba ya *NIDA*. Namba hiyo inaingia katika mtandao wa ajira, [tamisemi.go.tz](http://tamisemi.go.tz) kwenye taarifa

binafsi za mwombaji kwa mara ya kwanza. Mwombaji huyo akiwa hana namba ya *NIDA* hawezi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, vijana wetu wanaenda kukosa fursa ya ajira kwa sababu ya namba ya *NIDA*. Wakati anaomba kitambulisho cha *NIDA* alitumia cheti cha kuzaliwa ambacho cheti hicho na chenyewe ni vigezo vinavyohitajika katika maombi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba angalau kwa dakika 10 tu tuweze kupata muafaka wa suala hili, ili vijana wetu wasikose fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ameshatoa na haijaungwa mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walaizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Ameshatoa, ninyi ndio mlikuwa hamumsikilizi. Ametoa hoja na hakuna Mbunge aliyesimama.

Waheshimiwa Wabunge, Hata hivyo, hoja hii ya kazi ziliZotangazwa na Serikali na kigezo hicho cha kutaka namba za *NIDA*, sikumbuki vizuri ni mwaka gani, lakini kama miaka miwili hivi *TCRA* walikuwa wanasajili namba za simu na wakawa wana uhitaji wa hiyo namba ya *NIDA*. Kwanza, walisema kitambulisho, badaye wakasema namba; na watu wengi walipata hizo namba. Sasa sina hakika sana na ukubwa wa tatizo hilo kwamba nchi hii mpaka sasa hivi kuna mtu, acha kitambulisho, hana namba ya *NIDA*. Waziri yuko hapa. Kwa hiyo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walaizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muwe mnasikiliza. Nikisimama usianze kuropoka. Muwe mnasikiliza

hoja inaishaje? Muwe mnasikiliza. Usikivu ni muhimu na ni sehemu ya uongozi. Sikiliza wenzako wakiwa wanazungumza. Sawa sawa jamani! Eeh!

La pili, Kanuni ya 55 inaweka masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura. 55(1)(b), *“Masharti ya jumla yafuatayo yatatumika vilevile kuhusu hoja ya kujadili suala la dharura. Hoja zaidi ya moja katika kikao kimoja zenye kutaka kuahirisha Shughuli za Bunge kwa kutumia kanuni hii hazitaruhusiwa.”*

Sasa ukiisoma hii Kanuni ya 55, ya 54 na ile ambayo tulikuwa tunajadili hapa sasa hivi Kanuni ya 79 utagundua inataka mwendeshaji wa Bunge hapa mbele aangalie kama uendeshaji bora wa Bunge unaweza kuruhusu hayo mambo yote yafanyike. Sasa Waziri wa Nchi yuko hapa na ameshasikia hiyo hoja nzito kabisa kwa sababu, vijana wetu wanahitaji ajira.

Ikiwa kuna Wilaya mahali ambapo Ofisi za *NIDA* hazipo, moja; ya pili, hazina uwezo wa kutoa hizo namba katika kipindi hiki ambacho vijana wetu wanaajiri kazi, hicho kigezo maana yake Serikali mkiondoe kwa sasa; lakini kama ofisi za *NIDA* ziko kwenye wilaya zote na wanao uwezo wa kutoa hizo namba kabla ya muda wa kuomba hizi kazi haujaisha, basi vijana wetu wakapate hizo namba kwa sababu tunataka pia kuajiri Watanzania sio watu ambao wanatoka sehemu nyingine halafu wapate hizo kazi Serikalini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani hilo litakuwa limeeleweka vizuri. Mheshimiwa Waziri afuatilie hayo maeneo halafu nadhani tutawapa muda wao wangalie, kama kuna wilaya haina hiyo ofisi, hicho kigezo kwa sasa inabidi tu mkiondoe. Kwa sababu vijana wetu watakosa fursa ya ajira, lakini kama kila wilaya inayo, basi nadhani mwendelee na utaratibu mtoe hizo namba kwa haraka. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na hapa mbele ninayo majina mengi kabisa ya Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wametaka kuchangia kwenye hoja hii, lakini sasa kwa muda wetu uliosalia hatutaweza kuwa na Wabunge wengi wa kuchangia. Kwa hiyo, muwe radhi kwa sababu Wizara hizi huwa zinaleta bajeti zao kabla ya Bajeti Kuu, kwa hiyo, wengine watapata fursa kwenye Bajeti Kuu kwa sababu ile inazungumzia mambo yote ikiwa ni pamoja na ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwa hiyo, mtakuwa radhi kwa hao Wabunge wachache watakaopata fursa ya kuchangia.

Tutaanza na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Agnes Hokororo ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Afya...

**NAIBU SPIKA:** Kila Mbunge anayeitwa anachangia kwa dakika tano.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyenipa fursa hii ya kusimama kwenye Bunge lako hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye suala la ukosefu wa dawa kwenye hospitali zetu. Suala hili limekuwa ni tatizo kubwa. tunajua Serikali imejitahidi sana kwenye masuala ya miundombinu, lakini bado tuna

changamoto sana kwenye suala la ukosefu wa dawa. Akina mama wanateseka na watoto, wazee wanateseka. Nilikuwa naomba suala ambalo litamfanya Waziri wa Afya na timu yake nzima wasipate usingizi, wasilale usiku, ni suala la ukosefu wa dawa katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni suala la ukosefu wa dawa kwa sababu ya hujuma, labda wizi kwenye hospitali zetu, naomba hili suala kwa kweli; akina mama na watoto wanateseka, wazee wanakosa dawa na wagonjwa wengine wanakosa dawa hospitalini. Wale wanaoiba dawa hospitalini, basi mwaangalie na kuwaangazia macho sawa sawa kwa sababu katika jambo hili la ukosefu wa dawa kwenye hospitali, ni sawa sawa na kumsindikiza mgonjwa katika mauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anapokwenda hospitali na akakosa dawa, matumaini ya kuishi duniani tena hakuna. Kwa hiyo, nawaomba sana suala hili tuliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, suala la ukosefu wa madaktari, hili nalo ni changamoto kubwa. Watu wanapokwenda kwenye hospitali wanakosa madaktari, hii bado ni changamoto kubwa mno. Naomba Serikali kwa sababu imetangaza ajira hizo, iendelee kuongeza kasi kubwa kuhakikisha kwamba tunapata madaktari wa kutosha na manesi wa kutosha kwenye hospitali zetu ili kuokoa akina mama wajawazito na watoto na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wazee kupewa barua ya kwenda kupata dawa kwenye Dirisha la Wazee bado na yenyewe ni changamoto. Wazee hao wanateseka, hakuna dawa. Nilikuwa naomba Serikali iangalie hiyo Sera ya Wazee na yenyewe kwa sababu bado kuna changamoto kubwa, wale wazee wanateseka. Ni vizuri wakaja na mpango mahususi wa kuhakikisha kwamba wazee hawa badala ya kupewa barua kwa Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji, ni bora wapewe Bima ya Afya, hata kama ni hii iliyoboreshwa,

nao wapate iwe ni sehemu ya kuweza kuhakikisha kwamba wazee hawa wanaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, tuko hapa lakini tunapata matatizo makubwa kwenye majimbo yetu kwamba wananchi wanalia dawa hakuna, wazee wanateseka, watoto wanateseka, akina mama wanateseka, wajawazito na wagonjwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, naomba sana, sana sana Serikali yetu Sikivu ya Chama cha Mapinduzi, katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi chonde chonde; na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan alipokuja hapa Bungeni alituambia yeye ni mama, kwa hiyo, machungu ya mama anayajua vizuri. Kwa hiyo, naendelea kuiomba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ijitahidi sana katika suala la dawa; na Mheshimiwa Waziri usilale usingizi kwa sababu, wamama hawana dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali kama tuna majengo halafu hatuna dawa ni sawa na hakuna hospitali, lakini tukiwa na dawa; hospitali ndiyo dawa. Kama tukiwa na majengo hata maghorofa, kama hakuna dawa, hospitali hakuna; na unafuu wa maisha haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena kwamba suala la motisha kwa madaktari na lenyewe ni jambo ambalo Serikali ilianganilie kwa makini kwa sababu wale watu wanafanya kazi usiku na mchana, saa 24. Ni sawa na kazi ya jeshi. Wanajeshi wanafanya kazi usiku na mchana kama madaktari. Kwa hiyo, nawaomba pia suala la motisha kwa madaktari na manesi wetu ni suala la msingi na la muhimu sana ili waweze kuwa na moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado narudia kusema, suala la wizi wa dawa, lazima Waziri asilale usingizi kwa sababu kukosekana kwa dawa ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye matendo haya ya ukatili wanayofanyiwa Watanzania wenzetu. Kwa kweli inasikitisha sana ukiona Watanzania wenzetu na hasa akinamama na Watoto; katika takwimu ambayo Waziri ameisoma kwamba katika matukio 134,310 takribani matukio 106,196 wamefanyiwa akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hayo tu matukio, kuna matukio mengine yanafanyika huko wala hayarekodiwi popote, lakini jamii hii inaendelea kuteseka, inaendelea kuathirika kisaikolojia, wengine wanapoteza Maisha, wengine wanabaki na ulemavu wa maisha moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepita juzi huku Babati na maeneo mengine kuna kesi ambayo mpaka akinamama wa UWT wameishikia kidedea. Kwa mfano jana kulikuwa na kesi pale Babati ya mtoto katika familia mama ana watoto wake na mtoto wa ndugu yakem lakini imepotea shilingi 1,500 alichokifanya ni kuchukua shilingi 200 kuiweka kwenye jiko la mkaa ilivyokuwa nyekundu amemwekea yule mtoto mkononi yule anayetaka kumwadhibu, mkono umeungua, kesi ile imepelekwa polisi, bahati nzuri tumechangia kuwasafirisha wale. Matukio kama haya ni mengi, lakini kinachofanyika, kesi kama hizi ambazo tayari zina ushahidi baadaye watakubaliana zitakwenda kwa wazee, zitaongelewa zitakwisha, pamoja na kesi za ubakaji na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ku-*create awareness*, watu ambao wanaweza kuisemea wakahamasisha jamii sasa kutokomezwa kabisa ni hawa Maafisa Ustawi wa Jamii ambapo sasa wapo wachache. Wilayani utamkuta Afisa

Maendeleo ya Jamii au Afisa Ustawi yupo mmoja, kesi hizi ni nyingi, anashindwa kufuatilia, jamii inashindwa kuona wajibu wake. Naomba sasa Wizara hii kwa sababu kitengo hiki kipo kwao waongeze ajira ya Maafisa Ustawi wa Jamii, wafuatilie ili kwa pamoja tuweze kutokomeza matendo haya ya ukatili wanayofanyiwa Watanzania wenzetu pamoja na kuwasaidia vifaa vya usafiri na mengineyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia tena kwenye matibabu ambayo yanatolewa nchini kwetu. Kwanza ninaipongeza sana Wizara na Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kuna matibabu ya *dialysis* yalikuwa hayatolewa ndani ya nchi yetu, alikuwa mwathirika au mgonjwa anayetakiwa kutibiwa lazima asafirishwe kwenda nje. Kwa hiyo utaona kwamba ni familia zenye uwezo ndizo zilikuwa zinaweza kumsafirisha mgonjwa wake kwenda kutibiwa nje. Naishukuru Serikali kwamba sasa huduma hii inatolewa nchini, lakini ni katika maeneo machache, ni hospitali kubwa, kwa mfano matibabu haya yanatolewa Benjamin Mkapa, KCMC, Bugando na Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu hayo yanatolewa, mtu akishakuwa anatibiwa anatakiwa kwenda angalau mara mbili, tatu kwa wiki, kwa hiyo kinachofanyika familia yenye mgonjwa kama huyo kama anatibiwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa inabidi wahamie Dodoma wapate pa kuishi, lazima mwanafamilia mmoja akae na mgonjwa na kwa hiyo inaathiri familia nzima kiuchumi na kila kitu na isitoshe matibabu haya ni ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara sasa ni kwa nini sasa matibabu haya yasitolewe katika Hospitali zote za Mkoa ili kuwarahisishia Watanzania angalau wapate matibabu haya karibu na mikoani na Hospitali hizi za Kanda. Vile vile waangalie gharama hizi zipunguzwe. Najua kuna changamoto kubwa sana za wataalam wanaoweza kutoa matibabu haya. Namwomba Waziri husika wa Wizara hii awapeleke mafunzo Madaktari pamoja na wataalam ili tuwe na wataalam wengi wa kutosha na matibabu haya yaweze kupatikana angalau katika Hospitali za Mkoa.



Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho, naomba nichangie kuhusu bima ya Afya, watu wengi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele imeshagongwa Mheshimiwa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Amandus Chinguile, ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naamini wote tunatambua kwamba afya ni sehemu muhimu ya kuimarisha mtaji watu hasa katika kuendana na sera yetu ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwenye upatikanaji wa dawa. Kama ambavyo Mheshimiwa Noah amechangia na katika bajeti hii imeonekana ni asilimia 26.6 tu ndio iliyopokelewa kwa bajeti ya mwaka uliopita 2021. Hata hivyo, kinachokwamisha zaidi ukiacha ule utaratibu ambao ni wa ununuzi wa madawa kupitia *MSD* wa dawa nyingi yaani *bulk procurement* inaonesha pia kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya utaratibu wa manunuzi ndio hasa umekuwa kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vituo vya afya ama zahanati ambapo wakati mwingine wanakuwa na fedha, lakini katika utaratibu wa manunuzi inaweza ikachukua miezi miwili mpaka mitatu huku wananchi wanaendelea kuumia. Ikikupendeza katika Bunge lako hili Tukufu inawezekana kufanyike utaratibu wa kubadilisha hata sehemu ndogo ya Sheria ya Manunuzi ili kuwaokoa wananchi wengi wanaosubiria dawa wakati kwenye vituo vya kutolea

huduma ya afya hiyo ingewezekana, sio kwa kusubiri huo utaratibu wa miezi miwili mpaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika Mkoa wa Mtwara. Kama ambavyo taarifa imeonesha katika hotuba ya bajeti kwamba Kamati imebainisha wazi upatikanaji wa fedha katika bajeti iliyopita ndio ilikuwa kwa kiwango si cha kuridhisha, lakini natambua kabisa kwamba kwa bajeti ya mwaka huu 2021/2022, bajeti ya Wizara ya Afya imeongezeka kwa asilimia 31 na ongezeko kubwa limeonekana katika miradi ya maendeleo. Naiomba sana Serikali yetu sikivu ijielekeze pia katika kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara ambayo ni hospitali ya kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali hii ikikamilika itawanufaisha wananchi wa Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Lindi, lakini pia hata nchi jirani ya Msumbiji. Kwa sasa katika Mikoa hii ya kusini wananchi wote wanakwenda kufuata matibabu ya ngazi ya rufaa katika Hospitali ya Muhimbili, lakini Serikali ikikamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa inayojengwa pale Mtwara Mitengo ina maana hata mzigo ule wa Muhimbili utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba yale yaliyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi 2020 - 2025 inawezekana ikatekelezwa na iwapo Wizara itahakikisha hili inalitekeleza. Kwa sasa ujenzi wa hospitali hii umefikia asilimia 40, kwa hii miaka mitano naomba sana, kwa yale majengo tisa yaliyoanza ambayo kwa sasa kwa kweli inaonekana lakini haitawezekana kutoa huduma kama haitakamillishwa kama ilivyoelekezwa na Ilani ya chama changu Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Mtwara vituo vya kutolea huduma ya afya vipo 251 na katika hivyo tunazo zahanati 227 sawa na asilimia 22 tu, bado tupo chini na mahitaji ya zahanati yalitakiwa 985, lakini hadi sasa tunao ujenzi wa zahanati 28 ambao wananchi na halmashauri wamejitahidi. Naiomba Serikali ijitahidi kukamilisha haya maboma ili angalau haya 28 yakaongeze ile 227 na

wananchi kwenye maeneo mbalimbali waweze kupata huduma ikiwemo kule Lukuledi, ule ujenzi wa zahanati na ikiwezekana iwe kituo cha Afya Chiroro na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Chinguile na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wizara hasa Waziri na Naibu kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee hospitali yangu ya Mkoa wa Morogoro ambayo nilishaiongelea hapa ndani. Kwanza napongeza kwa upanuzi ambao wanaufanya kwenye hospitali hii ila ni upanuzi wa kwenda juu. Kwa hiyo sehemu ya hospitali ile kama wanavyojua Hospitali ya Mkoa wa Morogoro inapokea wagonjwa wengi hapo na majeruhi wengi sana, kwa hiyo sehemu hiyo haitoshi. Hapa nilishaomba kuwa kijengwe kituo au hospitali kubwa ya kisasa ya Morogoro ambayo inaweza ikapokea wagonjwa wengi na majeruhi wengi ambao huwa wanapokelewa hapo kutoka kwenye mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hospitali hii ni kubwa lakini haina *CT-SCAN*. Kutokana na matatizo yaliyo hapo nilishaongea na Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wakaniambia kuwa *CT-SCAN* ipo kwenye meli inakuja, sasa je, imefika wapi na itafika lini hapa hospitalini Morogoro au itakaa bandarini mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo kwenye Hospitali yetu ya Morogoro tunaloomba kutokana na umuhimu wa hospitali hii ni mtambo wa *oxygen* ambao nilishaongea na wenyewe, nikaambiwa kuwa nitaambatana

na Naibu Waziri aende kunionesha mahali pa kujenga hicho kituo cha mtambo wa *oxygen*. Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha hapa aniambie kwamba ni lini tutaambatana na Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri kwenda kuona hicho kituo cha *oxygen* kitakapojingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuliongelea kwenye Hospitali hii ya Morogoro ni wataalam Mabingwa, nalo naomba liweze kuangaliwa kwenye Hospitali yetu hii ya Morogoro ambayo inatibu wagonjwa wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimekumbana nalo, naomba nisisitize sana kuhusu upungufu wa dawa kwenye hospitali zetu na upungufu wa dawa kwenye vituo vyetu vya afya. Upungufu wa dawa kila mahali ni tatizo. Hata hivyo, nashukuru Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema viwanda vinajengwa vya kutengeneza dawa, basi naomba viangaliwe ili basi tatizo hili liweze kupungua kwa sababu limekuwa kubwa sana kwenye nchi yetu na kila mmoja anazungumzia upungufu wa madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye taarifa ya Serikali wanasema dawa zipo, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Doroth naye tuliongea mara nyingi kuhusu upungufu wa dawa, naye akakiri kweli kuwa atafuatilia upungufu wa dawa na wale wote wanaoiba dawa atawafuatilia. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba aliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo kwa uharaka naomba kulizungumzia ni Bima ya Afya. Unakuta mtu amelazwa *ICU* anaandikiwa dawa ya kutibiwa wakati yeye amelazwa, yaani anaumwa sana kwa sababu kupelekwa *ICU* ni kuwa unaumwa sana, lakini anaandikiwa dawa ambazo hazipatikani, inabidi eti uende kununua, inawezekana hiyo? Kwa hiyo naomba hiyo Bima ya Afya nayo iangaliwe, iendane na madawa yanayotolewa pia na Bima ya Afya kwa wote ijulikane ni lini itaweza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee utafiti, uangaliwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagoga Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana lakini utafiti ufanyike kwa magonjwa ambayo...

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa magonjwa ambayo...

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa magonjwa ambayo hayaambukizi yakiwepo kisukari, kansa, *pressure*, ugonjwa wa Ini na figo naomba utafiti ufanyike sio kutuambia kuwa hayatibiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Chinguile atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajjandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Nachingwea kwa namna wanavyonipa ushirikiano tangu wamenichagua kuwa Mbunge wao na nawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu kwa Wizara hii ya Afya. Tunayo changamoto ya watumishi wa afya, kwa mfano kwenye Halmashauri yangu ya Jimbo la Nachingwea, mahitaji ni watumishi 1,077 na waliopo ni 305, upungufu ni 772, hatuwezi kufanya kazi kwa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo nichukue nafasi hii kuwapongeza sana watumishi wa afya wa Jimbo la Nachingwea kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na upungufu wao huo. Mahitaji ya Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea ni watumishi 256. Mpaka sasa wako 169, sasa hawa 136 wanakwenda sasa kugawana kwenye zahanati 35 na vituo vya afya vitatu, haiwezekani! Niiombe sana Wizara kwenye hili waone namna watakavyokuja na mpango wa kutatua changamoto hii ya watumishi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Wizara walitujengea jengo zuri pale walituletea milioni zaidi ya 400 kwa ajili ya jengo zuri la Mama na Mtoto kwenye Hospitali yetu ya Wilaya ya Nachingwea. Pia walituletea milioni 200 kwa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Naipanga, nawashukuru sana. Pamoja na shukrani hizi jengo lile la mama na mtoto ni zuri, lakini mpango wake ni kupatikana kila Idara, Idara ya upasuaji jengo ni tupu halina kifaa hata kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Wizara na nimezungumza mara kadhaa na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wameniahidi, lakini basi angalau wakija kuhitimisha waseme lolote ili wananchi wale wa Jimbo la Nachingwea waweze kupata faraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo changamoto ya *ambulance*. *Ambulance* tunayoitegemea sasa ni ya Kituo cha Afya Kilimarondwa ambacho ni kilometa 96 kutoka kwenye Hospitali ya Wilaya. Ie *ambulance* ya wilaya pale ni mbovu haiwezi tena kuendelea na kazi. Sasa tufikirie kwamba *ambulance* inatoka kilometa 96 inakuja kutoa huduma katikati ya Wilaya ambapo ni umbali na barabara ni ya vumbi. Kwa kweli Wizara ione namna itakavyotusaidia kwenye Jimbo hili la Nachingwea ili na sisi tupate *ambulance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote niendeleo kuishauri Wizara, wenzangu wamesema hapa, sasa hivi tunalo ongezeko kubwa sana la magonjwa ya saratani na hasa ya shingo ya kizazi, lakini pia na magonjwa ya ini. Hebu tuone

namna ambavyo wataalam wanaweza kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha ongezeko la magonjwa haya kwa sasa ni nini, ili basi tuweze kutoa elimu kwa wananchi wetu na kwa hiyo tutapunguza wagonjwa wanaohitaji sasa kupata huduma kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze zaidi kwenye magonjwa ya *malaria* kipindi kilichopita tullendelea kutoa elimu kubwa sana kwenye magonjwa haya kupambana na ugonjwa huu wa *malaria*. Sasa ni kana kwamba tumepunguza *speed*, niombe Wizara turudi, kulikuwa na mipango hapa ya kugawa neti na vitu vingine, ile mipango bado iwe endelevu. Yapo maeneo ambayo kama hatutapeleka elimu ya kutosha bado wananchi wetu ni kana kwamba wanasahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq, tutamalizia na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Najua muda ni mchache sana lakini nitajitahidi. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa maandalizi ya bajeti hii, lakini sambamba na hilo naomba nitoe ushauri kwamba, pamoja na kwamba Serikali imeweka vipaumbee vyake katika Fungu la 52 pamoja na Fungu 53, naomba nitoe ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la kuimarisha huduma ya chanjo, naomba niishauri Serikali kwenye hii *issue* ya chanjo ya ugonjwa wa ini ni kwamba chanjo hii ili ukitaka kuchanja inabidi utoe shilingi 20,000 pale unapokwenda kupima halafu baadaye inabidi utoe Shilingi 10,000, Shilingi 10,000, Shilingi 10,000 kwa ajili ya dozi. Naomba Serikali ione ili kusudi wale wananchi wa pembezoni waweze kuweza kuchanja chanjo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka nizungumzie kuhusiana na wanawake ambao wanakwenda kujifungua. Taarifa zinaonesha kwamba imeonekana kwamba wanawake wengi wanajitahidi kwenda kujifungulia kwenye kliniki na hospitali, lakini bado kuna wale wachache ambao bado wanajifungua kwa waganga au wakunga wa jadi. Nashauri elimu iendelee ili kusudi watoto wawe salama na akinamama wawe salama, ni vizuri wakaenda kujifungulia katika hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nizungumzie suala la magonjwa ya kuambukiza ikiwemo Malaria, Kifua Kikuu na hasa UKIMWI nijikite zaidi kwenye UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi sana wamezungumzia kuhusu hili suala la UKIMWI na inaonyesha kabisa kwamba kundi kubwa ambalo liko kwenye hatari ya kuambukizwa UKIMWI ni hawa Watoto kuanzia miaka 14 mpaka 24. Takwimu zinaonyesha kwa mfano katika Mkoa wa Njombe kwamba maambukizi yako kwa asilimia kama 11.3 kwamba hawa Watoto wenye umri kati ya miaka hiyo 14 na 24 katika wale vijana 10 wanaopimwa wa kike wanaonekana kwamba wanamaambukizi makubwa sana.

Kwa hiyo, ina maana kwamba Watoto wa kike 8wanapata maambukizi katika 10. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri akinababa hebu muwaonee huruma hawa Watoto, kwasababu inaonekana kwamba mmeacha kwenda kwa akinamama watu wazima mnawafuata hawa Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa wale wa baba ambao wanakwenda kuwadanganya hawa Watoto hebu waacheni hawa Watoto hebu waacheni hawa Watoto wasome wafikie malengo yao. Kwa hiyo nilikuwa naomba nishauri. Lakini sambamba na hilo wenzangu wamezungumza kuhusiana na suala zima la kwenda kupima UKIMWI tunaendelea kuhamasisha wanaume waende wakapime Ukimwi kwasababu kama hawa Watoto wa kike wadogo



wanakuwa hawana maambukizi haya maambukizi mapya wanayapata wapi? Ina maana kwamba wanayapata kwa wale akina baba ambao hawajapima Ukimwi. Kwa hiyo nilikuwa naomba nishauri kwamba akina baba bado waendelee kujitokeza kupima Ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo jingine nililokuwa nataka kuzungumzia ni kuhusiana na huduma za uzazi wa mpango. Ni kwamba inaonyesha kwamba katika hotuba imeonyesha kwamba katika hotuba inaonyesha kwamba kuanzia Julai 2020 hadi Machi, 2021 inaonesha takwimu za akinamama ambao wamepata uzazi wa mpango ni 4,926,183 kati ya akinamama 13,841,830 sawa na asilimia 36. Hii bado ni asilimia ndogo kwa hiyo nilikuwa naiomba Serikali pia iwekeze sana kwenye suala zima la uzazi wa mpango ili kusudi tuweze kupanga mipango yetu ya maendeleo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa naomba nizungumzie kuhusiana na huu mpango kazi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na Watoto MTAKUWA wa mwaka 2017 hadi 2018, 2021/2022. Najua azma nzuri sana ya Serikali kwa ajili ya mpango huu nikuhakikisha kwamba ukatili unapungua au unakwisha kabisa. Lakini tatizo linakuja kwamba hivi vikundi vya MTAKUWA katika ngazi ya vijiji na kata havipati pesa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ione Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI washirikiane kuona kwamba zinapangwa bajeti ili kusudi huku katika ngazi za vijiji na kata vikao hivi viweze kukutana kuweza kufanya mikutano yao ili kupinga suala zima la ukatili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda siyo Rafiki...

**NAIBU SPIKA:** Imeshagonga kengele Mheshimiwa.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareeso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na niweze...

**NAIBU SPIKA:** Utafatiwa na Mheshimiwa Mwanaidi Hamis.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze jambo la kwanza kuhusiana na kampeni ya usafi wa mazingira kitaifa, kampeni hii ilikuwa inafanywa na wadau muhimu ambao walikuwa na *slogan* yao ya nyumba ni choo. Mradi huu uliendeshwa kwa kuijenga jamii kuelewa namna bora ya kuwa na vyoo bora lakini kunawa mikono na kuhakikisha kwamba wanakuwa na vyoo vinavyotumika kwenye kila kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hii ilikuwa ina ufanisi mkubwa sana kwasababu imezunguka kwenye mikoa 18 na matokeo yake ni kuongezeka kwa kaya zenye vyoo bora kutoka asilimia 39 mwaka 2017 hadi asilimia 67 mwaka 2021. Haya ni mafanikio makubwa, lakini pia kampeni hii inasaidia mwisho wa siku kuibadili jamii kitabia na kimienendo lakini inasaidia kuweka kinga kwenye jamii ili kusiwepo na magonjwa mbalimbali ya maambukizi ambayo yanatokana na ukosefu wa vyoo katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi ni vyema Wizara natambua mradi huu unaisha na mradi huu ulikuwa *funded* na Wizara basi ni vema Wizara ikaendelea kuwekeza kwenye kampeni hii ambayo itaendelea kuisaidia jamii kujiandaa kukabiliana na magonjwa mbalimbali lakini kuwa na vyoo bora kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni hii mwisho wa siku inasaidia hata katika magonjwa mbalimbali ya milipuko kama Corona na mengine ambayo hatujui kama yatakuja au hayaji kuisaidia jamii kuiandaa katika ustawi bora Zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuna hii dawa ya *Phyt Exponent*, ninaushahidi imesaidia kwa mtu ambaye alikuwa anaumwa corona lakini wako wengine ambao walikuwa wanaumwa kansa imeonyesha matokeo bora na mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa dawa hii ni ghali na upatikanaji wake kwa watu wa kawaida siyo rahisi inauzwa 150,000 sababu za kuuzwa 150,000 kwasababu haijasajiliwa kama dawa tunaiomba Wizara kwasababu imeshathibitishwa na Mkemia Mkuu wa Serikali, na imeshaonyesha matokeo na hata hivyo mtu anapougua mwisho wa siku imani ya mtu kutokana na anachokitumia kinasaidia kuponya, watu wanaimani na hii basi tunaomba Wizara isajili hii *diet Supplement* ili iweze kupatikana kwa urahisi na kwa unafuu na iweze kusaidia jamii yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni Idara ya Maendeleo ya Jamii Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ina watu wa Ustawi wa Jamii na Watu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. Watu wa Ustawi wa Jamii ni muhimu sana kwenye jamii yetu na watu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana kwenye jamii yetu kwasababu inaiandaa jamii kukabiliana na changamoto mbalimbali lakini inaleta chachu ya maendeleo katika jamii kwa kuihamasisha jamii. Lakini Idara hii sina hakika kama Wizara na Serikali kwa ujumla mnaona umuhimu wa Idara hii na kuhakikisha kwamba kunakuwa na rasilimali watu wa kutosha katika idara hii ili isaidie jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mahitaji ya watu ustawi wa jamii ni 22,000 lakini walioajiriwa ni watu 744 kwa hiyo kuna ajira iliyotolewa walioko kazini Maafisa Ustawi wa Jamii ni asilimia 3.2 ya uhitaji wote wa nchi nzima hiki ni kiwango kidogo kabisa. Ni vema Serikali ikaweka umuhimu kwa kuhakikisha tunaajiri maafisa ustawi wa jamii wa kutosha hawa maafisa ustawi wa jamii wa kutosha wakipatikana ndivyo ambavyo tutajenga jamii yetu kimaadili tutachochea maendeleo, tutahakikisha ukatili tunaouongelea kila siku

ukatili wa watoto, ukatili wa kijinsia, mambo mengi yanayoendelea katika jamii yetu kama tuna watu kama hawa wa kutosha kwenye halmashauri zetu tutahakikisha tunakuwa na jamii yenye ustawi yenye amani yenye kuwa na maendeleo ambayo tunayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hoja yangu ya mwisho upungufu wa watumishi katika sekta ya afya, takwimu zinaonyesha kuna upungufu wa watumishi wa afya ni asilimia 53 sasa kama tutakuwa tunajivunia tunajenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya tunaimarisha hospitali za kanda tutabakiwa na majengo yasiyokuwa na watumishi wa kutoa huduma muhimu za afya kwa watu wetu. Tunataka Serikali muwe na mpango sambamba mpango wa kujenga zahanati zetu vituo vya afya na hospitali za wilaya uendane na mpango wa kukajiri watumishi kuhakikisha watumishi wanapatikana wakutosha watanzia wanatamani kupata huduma iliyobora ya kutosheleza na ya uhakika kwa kuwa na watumishi wa afya wakutosha ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanaidi Hamis Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuniwezesha kuwepo hapa kujibu hoja ambazo zimechangiwa na Wabunge pamoja na Kamati ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikushukuru wewe kwa kutuongoza pia nimshukuru Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitaua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto nikiwa kama mama basi sitamuangusha katika kutekeleza na kumsaidia majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Dkt Philip Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiongoza na kutuongoza katika nchi yetu. Kipekee nimshukuru Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii Dkt Dorothy Gwajima kwa upendo na ushirikiano wa hali ya juu ambao amekuwa akinipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze kamati ya kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa michango yao mizuri na maoni yao waliyotupa tutajitahidi kuyazingatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wote wananchi wa Chama cha Mapinduzi pia niwashukuru watanzania wote niwape pole watanzania wote kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kujibu hoja za kamati ya kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Serikali kutoa ajira kwa maafisa wa jamii na maafisa wa jamii kuwa katika vyo vyetu vilivyoanzishwa na wataalamu hawa kutosha kuwepo wakiwa hawana ajira. Wizara imepokea ushauri wa Kamati.

Aidha Wizara inaendelea kushirikiana na TAMISEMI pamoja na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kutatua changamoto za upungufu wa maafisa wa maendeleo ya jamii maafisa ustawi wa jamii katika ngazi za mamlaka za Serikali za Mitaa kadri bajeti ya Serikali itakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo kwa vyo vya maendeleo ya jamii kuongezwa lakini pia fedha zilizotengwa zitolewe zote kwa wakati hasa kuzingatia vyo hivi ndivyo vinavyotegemewa kuanzisha maafisa maendeleo ya jamii ambao ndio nguzo muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetoa ushauri kwa kamati aidha, mwaka 2021/2022 Wizara imeandaa fedha kiasi cha shilingi milioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa ukarabati wa maendeleo na miundombinu ikiwemo kumbi za mihadhara mabweni, maktaba na majengo ya utawala katika vyuo vya maendeleo kwa jamii ya Ruaha shilingi milioni 600, Rugemba shilingi milioni 500, Uyole shilingi bilioni moja na Mlale shilingi milioni 500 na Monduli shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itafanya kazi kwa utaratibu na kuhakikisha kwamba fedha hizo zilizotengwa kwa mwaka 2021/2022 zitatolewa kwa wakati ili kutekeleza kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya kuwezesha utekelezaji wa mipango kuzuia ukatili wa kijinsia kutengwa na kutolewa wakati badala ya kutegemea fedha za nje. Wizara imepokea ushauri wa kamati kwa mwaka 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 791 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali za kutokomeza ukatili wa kijinsia. Wizara itaendelea kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kulingana na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika kujibu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndimbo Mbunge wa Viti Maalum kuhusu vituo vingi vya wazee kuwa nje ya mji na vinahatarisha maisha ya wazee kutokana na kuwa mbali na vituo vya afya. Pia kuhusu huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya wazee kupata huduma ya kwanza tu ambazo hazivasaidii wazee wanaoishi katika vituo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia na kutoa huduma kwa wazee katika makazi 13 inayomilikiwa na asilimia kubwa ya makazi hayo yapo mjini. Mfano Fungafunga ambayo iko Morogoro Manispaa ya Morogoro, Ipuli Tabora Manispaa, Nunge Kigamboni, Njoro Moshi Manispaa, Magugu Babati Mjini, Kalandoto Shinyanga Manispaa, Makumbi, Misingwi, Mwazange Tanga Jiji, Nyambange Musoma Manispaa, Kilima Bukoba Manispaa na Kibirizi

Kigoma Manispaa. Makazi yaliyo nje ya mji ni Muheza na Sukumahale Singida hata hivyo Serikali imeandaa kuisimamia huduma hizi kuhakikisha uwepo wa wahudumu wa afya katika makazi ya wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kutokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya wazee na halmashauri ikiwemo vituo vya afya katika maeneo ya makazi yaliyopo upatikanaji wa huduma hizo zimeimarishwa. Hata hivyo juzi mimi katika ziara yangu toka nilipochaguliwa nimetembelea Kituo cha Nunge na kuona wazee wako vizuri sana na niliwauliza wahudumu wa afya wakaniambia wanapatiwa huduma zote dawa zipo hawana wasiwasi na wanashukuru sana Mheshimiwa Rais wao Mama Samia Suluhu Hassan kwa kumteua mwanamke ambaye ataendeleza kuwalea Wazee wale kwa kushirikiana na Serikali ambayo ya Awamu ya Sita inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ritta Kabati Viti Maalum Watoto saba waliobakwa na mwanaume mmoja kati ya Mkoa wa Iringa Serikali iangalie sheria kulinda Watoto hawa. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu unaofanywa na masuala ya haki ya ustawi wa jamii ya mtoto tumeipokea taarifa na ufuatiliaji kama sehemu ya utekelezaji wa Wizara kupitia MTAKUWA.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ili kuhakikisha haki zote zinalindwa Serikali imeongeza idadi ya mahakama za watoto kutoka mahakama tatu mwaka 2015/2016 hadi kufikia mahakama 147 mwaka 2021.

Pia Serikali itaendelea kuratibu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa mashauri ya watoto mahakamani. Kupitia maafisa utawala wa ustawi wa jamii vilevile Serikali inaendelea kuimarisha dawati la jinsia la Watoto katika vituo vya Polisi ambapo hadi kufikia Aprili 21 madawati 420 yameanzishwa nchi nzima ili kuhakikisha mashauri ya Watoto yakiwemo ubakaji yanasimamiwa kwa umakini kwa lengo la kulinda haki za Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tokea niteuliwe nimeamua kuandaa mikakati ambayo tutashirikiana na TAMISEMI na Mahakama na Ofisi ya Mambo ya Ndani ili kuweka mikakati hii ambayo kukomesha ukatili wa watoto katika nchi yetu, na suala hili tutapita halmashauri zote katika mikoa yote ya Tanzania kuelimisha suala hili ambapo mikakati yetu itakapokuwa sawa Waheshimiwa Wabunge nakutakeni muwe ni walezi na kutoa ushauri na hoja ambazo mtakazozitoa katika kuelimisha wananchi maana nyinyi kama mliyoweza kuwahadaa wananchi wakakupeni kura mkafika hapa nafikiri na nyinyi ni rahisi kuwahadaa watu hawa...

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lembris.

#### T A A R I F A

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri ametumia lugha ambayo kidogo ina washushia Waheshimiwa Wabunge hadhi au Bunge hili kwamba tumewahadaa wananchi kuwadanganya ili waweze kutuchagua hivyo ningepomba atumie lugha ya staha au arekebishe kauli yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani ulikusudia kusema kuwashawishi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nimepokea hoja nilikusudia kuwashawishi lakini katika kutekeleza na kuhamasisha wananchi imenibidi nitumie hoja ya haraka haraka kuwahadaa samahani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu nakuombeni mikakati ambayo tutakayoipanga mtusaidie kwa wananchi kuwahamasisha ili kutokomeza ukatili katika



nchi yetu na mimi nitakuwa pamoja *time* yoyote wakati wowote na tutatoa matangazo na namba za simu mikoa yote hadi vijijini ili likitokea suala hili niweze haraka kusimamiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawatahadharisha ambao Wakurugenzi mahakama ma-*DPP* ambao wanadhorotesha kesi hizi tutakuwa sambamba, mtu ambaye tutamgundua anadhorotesha kesi hizi basi hatua za haraka tutazichukua ama kumuhamisha kumuweka mtu mwingine ili ukatili huu uondoke hapa nchini. (*Makofi*)

Kuhusu hoja ya Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ambayo inahusu kuandaa namna bora ya kuwapatia watoto yatima walioko kwenye vituo hati za kuzaliwa ili ikiwezekana waanze shule huku ufuatiliaji wa hati zao ukiendelea. Kuhusu watoto yatima wasio na vyeti vya kuzaliwa naomba nipokee ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

Aidha, Wizara itaendelea kuwasiliana na *RITA*, *TAMISEMI* pamoja na Wizara ya Elimu, Sanyansi na Teknolojia ili kuhakikisha kuwa watoto yatima wote kwenye vituo wanapatiwa vyeti vya kuzaliwa na kuendelezwa kielimu ili kupata haki yao ya msingi mpaka hapo watakapoanza kujitegemea wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Norah Mzeru aliongelea suala la wanawake kukumbukwa katika masuala ya afya na kuwawezesha kiuchumi ili kuweka mazingira bora kuanzia ngazi ya halmashauri. Serikali inaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia programu mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (*MTAKUWWA*). Kupitia mpango huu, Serikali imewezesha wanawake kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu katika Benki ya *TPB* na asilimia nne ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inaendelea kuwaunganisha wanaweke wajasiriamali na taasisi kutoa

mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kibiashara wa usindikaji wa bidhaa na matangazo ya biashara kwa njia za mitandao. Halikadhalika, Serikali inawawezesha wanawake wajasirilimali kushiriki maonesho ya kibiashara ya Sabasaba na Nanenane, program za uwezeshaji wanawake kiuchumi na makongamano ya kibiashara ili kujua mahitaji ya masoko ya bidhaa zao. Hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza afua na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, anauliza Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha wazee wanapata Bima ya Afya. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na zoezi la uchambuzi wa wazee ili kuwapatia vitambulisho vya matibabu. Hadi kufikia Machi 2021 jumla ya wazee wanaume 1,834,995 na wanawake 1,002,567 wametambuliwa ambapo wazee wasio na uwezo 1,042,403 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo. Aidha, Serikali inaendelea kukamilisha rasimu ya Muswada ya Bima ya Afya kwa wote wa mwaka 2020 ili kuwawezesha wananchi wote wakiwemo wazee kupata huduma za matibabu kwa mfumo rasmi na ulio mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja na kuwapongeza Wabunge wote waliotoa hoja zao katika kurahisisha utendaji wa Wizara yetu ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Nawashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, karibu kwa mchango wako, tutamalizia na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama hapa, kwanza nimshukuru Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini tena na

kuniteua kuendelea kumsaidia katika eneo hili la afya. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *mentoring* nzuri anayotufanyia wakishirikiana na *Chief Whip*, Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama ambapo kwa kweli imetusaidia sana kurahisisha shughuli zetu. Pia nikushukuru wewe na Mheshimiwa Spika kwa ushirikiano mzuri ambao mnatupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kabla ya kuanza, niseme tu kwamba sitaweza kuwataja kwa majina wote waliochangia lakini wakati Waziri atakapohitimisha ataonyesha michango yenu na wote waliochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kujibu hoja za Kamati ambapo kimsingi zimefanana na zimegusa yale ambayo vilevile yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya kwanza ilikuwa ni kuhusu kuongezeka kwa bajeti kwenye eneo la akina mama na watoto ili kupunguza vifo vyao. Katika eneo hilo Wabunge wengi vilevile wamechangia lakini utaona kwa bajeti ya mwaka 2021 ilikuwa ni shilingi bilioni 55 na sasa imeongezeka imefika shilingi bilioni 63. Maana yake kuna ongezeko la bilioni kadhaa hapo ambazo sasa zinaenda kuongeza nguvu kwenye yale maeneo ambayo yanaenda kutuongezea kasi kwenye kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Pia utaona vituo vya kufanyia upasuaji kwa maana ya kupasua kutoa mtoto tumboni vimejengwa 304 na tayari vifaa tiba kwa ajili ya upasuaji huo vimeshawekwa kwenye vituo 238.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hilo Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, amezungumzia upandikizaji wa mimba. Tumelichukua jambo lake ambalo kwa kweli kwenye kutengeneza Bima ya Afya kwa Wote, lakini kwenye ongezeko hili la bajeti na eneo hilo linaenda kuongezwa nalo

ili kuchukuliwa uzito ambao Mheshimiwa Mbunge amezungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Dkt. Thea na Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu walieleza suala la tohara kwa akina mama ambalo nalo hili linaongeza vifo vya akina mama. Waziri wetu anapouliza wanaume mpo huwa anataka tuelekeze nguvu kwenye eneo hilo, tu-*address* magonjwa yanayotuhusu sisi wanaume na yale ambayo yanaumiza akina mama ambapo sisi tunaweza tukawa *solution*. Sisi Wabunge tunaotokea maeneo yenye changamoto hiyo kama Umasaini au Ukuriani ambapo hali ni mbaya zaidi tuungane na tutengeneze utaratibu wa pamoja tukaenda kuhamasisha na sisi tukawa watu wa kwanza kulizungumzia hilo kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ya Kamati ambayo vilevile Wabunge wengi wameizungumzia ni suala la watoto njiti. Kamati ilizungumzia hasa Muhimbili lakini utaona kuna upanuzi walikuwa na vitanda 66 tu lakini sasa vimeongezwa vimefika 130. Vilevile ukiangalia Muhimbili kwa mwaka akina mama wanajifungulia pale ni 54,000, lakini watoto njiti kati ya hao 54 ni 14,400.

Kwa hiyo, hapa ili tuweze kutoka vizuri eneo hili Serikali imeongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 37.8 hadi shilingi bilioni 52.2. Pia ongezeko la bajeti ya shilingi bilioni 55 hadi shilingi bilioni 63 nalo linaenda ku-*address* eneo hili na kutatua tatizo ambalo linasababisha yatokee matatizo ambayo Wabunge na Kamati yetu imeyaainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limeibuka ni eneo la Bima ya Afya, wengi wamezungumzia matatizo yalioko kwenye eneo hili. Vilevile Kamati imeshauri suala la ushirikishwaji kwamba kabla ya kuleta Bima ya Afya kwa Wote hapa Bungeni wananchi na wadau mbalimbali washirikishwe. Serikali imechukua ushauri huo na kabla ya Muswada huo kuja hapa Bungeni wadau wote watashirikishwa kuanzia wananchi na watu wengine wowote ambao utawagusa na tunaamini na ninyi kama sehemu

muhimu sana mtaingiza *input* ambazo zitaondoa matatizo mengi yaliyoko kwenye Bima ya Afya iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Kamati imelizungumzia lakini na Waheshimiwa Wabunge pia wamegusia ni kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye suala la Bima ya Afya. Sisi tunasema wakati Muswada huu utaletwa Bungeni mtaona umeweka kipengele ambacho kinaruhusu sekta binafsi kushiriki kwenye eneo la bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuja ni wateja wa *NHIF* kukosa huduma lakini likagusiwa suala la *CHIF*. Tulichokuja kugundua wakati tunasikiliza kwa makini kuna wakati watu wanachanganya wanasema bima akimaanisha *CHIF* na wakati mwingine anasema bima akimaanisha bima ya afya ile kubwa ambayo inatolewa kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoweza kusema hapa ni kweli tatizo hilo liko na linasababishwa na upungufu wa madawa kule chini. Ukienda kwenye eneo la *CHIF* wananchi wamehamasishwa sana kukata zile kadi zao lakini wanapokuwa na kadi zao wanapokwenda kwenye dirisha la dawa wanakuta hamna dawa, kwa hiyo, thamani ya ile kadi aliyoikata inakosa maana. Tumeenda baadhi ya maeneo kwenye wilaya hata wananchi wenye bima hii ya afya kubwa kama walimu hata wafanyakazi wa afya wanapokuwa maeneo remote huko vijijini wakikosa dawa kwenye vituo vyetu na hakuna duka lenye dawa zote kwenye eneo lao inabidi asafiri kilometa nyingi ambapo anatumia shilingi 10,000 kufuata dawa ya shilingi 3,000. Tunachosema wakati tunakuja kwenye Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, lakini wakati tunaelekea kwenye kuboresha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu haya matatizo yote yataenda kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni eneo la Corona. Watu wengi wamezungumzia Corona na ni namna gani tunafanya. Kwanza, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu kwanza kuna Kamati ya Rais ambayo

inafanya kazi hiyo na inatoa ushauri mzuri sana kwa Serikali na hilo linaendelea vizuri. Hakuna kitu kipya hapa ambacho kimeanzishwa kwa sababu kama mnakumbuka Mheshimiwa Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli akiwa Kagera alitushauri Wizara ya Afya msipokee vitu, lakini msifanye vitu bila kufanya upembuzi yakinifu. Hicho ndicho anachoendeleza Rais wetu wa sasa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameunda Kamati Maalum ambayo itaangalia kwa umakini ni nini kinaingia na nini kinafanyika kwa ajili ya usalama wa watu wetu. Mheshimiwa Rais ameendeleza umakini kwenye hilo hilo na Kamati hiyo inashauri vizuri sana kuhakikisha mambo ambayo tunaenda kufanya ni yale ambayo yataboresha usalama wa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Gwajima amesema jana kwa uchungu mkubwa sana na hasa akitilia hofu kwenye eneo la chanjo. Amezungumzia chanjo za *RNA* na *DNA* na ameuliza chanjo zingine ni vitu gani. Ukweli ni kwamba Serikali inajua na ndio maana kuna Kamati Maalum ya wataalam yenye Maprofesa na watu wengine waliobobea na wanajua kwamba kuna hizo chanjo za *RNA* na *DNA*. Zile za *RNA* zinaingia kwenye seli lakini zinasemekana haziendi kwenye *nuclears* kwa maana ya kugusa *DNA*. Hata hivyo, watu wetu wanaangalia ukweli huo ni wa kiasi gani kabla sisi hatujasema lolote ndio maana ya timu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna zile ambazo ni za *DNA* ambapo wametumia *adenovirus* ambao ni *virus* kutoka kwenye chimpanzee, wanachukua *DNA* ya *virus* wa *Corona* halafu wanachanganya na *adenovirus* ambayo ni *type 5* unakuta katikati kuna *virus* huyo wa *Corona* pembeni na pembeni kunakuwepo na *DNA* ambayo anatokana na *adenovirus* ndiyo anaingizwa mpaka kwenye *nuclear* halafu baadaye anatengeneza hizo protini. Ndiyo kazi ya Maprofesa wetu na Rais ameelekeza nguvu zote pale ili wajihakikishie hiyo *adenovirus* na vitu vingine haina matatizo mengine? Kwa sababu tunajua *genetic makeup* moja hai-present kitu kimoja, unaweza ukasema unataka kutengeneza protini hizi lakini kumbe hiyo sehemu ilikuwa na uwezo wa kutengeneza protini zingine ambazo zinaweza zikawa na madhara kwa

watu wetu. Timu hiyo ndiyo inafanya kazi hiyo kuhakikisha tunajibu maswali haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwahakikishie kabisa Serikali ya Tanzania haibishani na dunia au *WHO*, wala Tanzania haijioni yenyewe ni kisiwa, inakubaliana na mambo yote yanayotokea kisayansi na afya katika dunia. Ubishani hauko kati ya Serikali au Wizara na mtu yeyote, ubishani uko kati ya wanasayansi kuhusu usalama wa kitu tunachoenda kufanya. Kwa hiyo, huo ni ubishani sio kutofautiana, hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaulizana kisayansi unaposema hiki kinaingia kwenye *cell* hakikuzi *DNA*, ukizingatia tunajua kwenye eneo la mimea (*Genetic Modified Foods*) wakati fulani mapapai yalikuwa *modified genetically* yakatoa mapapai mwaka wa kwanza baada ya miaka miwili yakatolewa mapapai lakini hayana mbegu. Kwa hiyo, sasa tunajuliza haya maswali, je, kwa binadamu usalama uko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tukubaliane kwamba dunia inakoelekea mwisho wa siku chanjo nyingi baadaye zitakuwa zinatengenezwa na *RNA* na tunaenda kwenye *genetic therapy*. Kwa hiyo, hatuwezi kubishana na dunia na sayansi iliyopo, anachofanya Amiri Jeshi wetu Mkuu ni kwamba hata kama tunakubaliana na dunia tuhakikishe tuko salama kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kwenye tiba ya asili, Wabunge wengi wamezungumzia eneo hili na tumechukua mawazo yao yote. Mpaka sasa wataalam wa tiba asili na tiba mbadala 27,793 wameshasajiliwa, vituo 1,003 vimesajiliwa, dawa 49 zimesajiliwa lakini mafunzo yamefanyika kwa wataalam wa tiba asili 335.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kwenda mbali zaidi ndiyo maana utaona Serikali yetu imepeleka fedha *NIMR* kwenye sehemu ya utafiti, hatutaki tu kuishia kusema huu mti unatibu, unaupika huo mti halafu unapata *juice* yake halafu

unakunywa, tunataka watu wa *NIMR* wakae chini wajue ndani ya huo mti ni *molecule* gani ziko ndani yake ambazo ndiyo zina sifa ya tiba. Pia hizo *molecule* ziwe *extracted* vitu vingine vinatupwa tunaanza kutengeneza *syrup* na vidonge, huko ndiko tunakotaka kuelekea. Kama mnavyojua *quinine* inachukuliwa kwenye magome ya miti inaenda nchi zingine mwisho wa siku inatolewa kile kinachotibu inarudi kama sindano tunakuja kutibiwa hapa malaria. Kwa hiyo, tunataka tufike kwenye sayansi kubwa na ndio muelekeo wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la *CCBRT* kusajiliwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30, kengele imeshagonga.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari *CCBRT* imesajiliwa, hivyo, agizo la Kamati limeshatekelezwa. Tunatambua mchango mkubwa unaofanywa na *CCBRT* na Kamati ilitembelea kwa kweli Mkurugenzi wa *CCBRT* anafanya kazi kubwa na sisi kama Wizara tutampa ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimuite mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi wakati wa uwasilishaji wa hotuba yangu.



Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge aliyewasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2021/2022 na kuipongeza Wizara yangu, nasi tunamshukuru kwa kututia moyo. Pongezi hizo nimezipokea kwa niaba ya watumishi wetu wote wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge 34 waliochangia jumla ya hoja 57 katika hotuba yangu ambapo Waheshimiwa Wabunge 29 wamechangia kwa kuzungumza na wengine wameendelea leo ambao tumewarekodi kama sita na Waheshimiwa Wabunge watano wamechangia kwa maandishi. Nina imani kwamba wengine bado wanaendelea na tutuzidi kuzipokea na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba pia niwashukuru na kuwatambua waliochangia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge ambao ni Waheshimiwa Wabunge 26 ambapo pia tumepokea michango yao na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru sana Manaibu Waziri wangu wote wawili kwa michango yao mizuri waliyoitoa kujibu hoja hizi kama utangulizi, kabla sijaendelea sasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni nyingi, nzuri zina tija, zina mashiko na zinafaa kufanyiwa kazi; na nyingi zinaweza kufanyiwa kazi vizuri kabisa pasipo hata kuwa na gharama kubwa sana, tukaweza kuleta mabadiliko. Wametufungua mawazo, wametutia moyo, nasi tunaahidi kwamba tumepokea. Mimi mwenyewe nilikaa hapa jana nikaandika sana, nina kila kitu, kama tutaweza kuwasilisha kwa maandishi wataona kwamba kila mmoja tumemtendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu michango ni mingi; na kwa sababu yote ni ya muhimu; na kwa sababu muda unaweze usitoshe naomba nijielekeze kwenye maeneo makubwa ambayo wengi sana yamewagusa, naamini hata ambao hawakuchangia kwa kuongea au kwa maandishi, itakuwa hizi zimewagusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni masuala mazima ya dawa.nikimaliza hapo nitakwenda kwenye masuala ya upatikanaji wa watumishi; nikitoka hapo nitagusia masuala ya CAG na MSD kuhusu masuala ya Covid kupitia uzalishaji wa PPE, (Personal Protective Equipment), uliweza ukafanyika na ufafanuzi wake ni upi? Nitagusia kidogo kuhusu miradi ya ujenzi wa hospitali na tunahitaji na hospitali hizi zikamilike ili Muswada wa Sheria ya Bima ukute huduma zinapatikana. Muda ukiniruhusu nitakwenda kwenye maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uhaba wa dawa, iliripotiwa kwamba kutoka kwenye hoja za Kamati. Hii imezalishwa na hoja za Kamati, lakini pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa mdomo nao wamesema. Kuhusu uhaba wa dawa nchini iliwasilishwa kwamba katika mwaka wa 2021kiasi cha shilingi bilioni 200 kilihidhinishwa na Bunge kwa ajili ya dawa lakini hadi kufikia Machi, 2021 ni asilimia 26 tu ya fedha hizo zilikuwa zimetolewa. Hivyo bajeti inayoidhinishwa na Bunge iwe inatolewa kikamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inakiri kwamba mwaka huu 2020/2021 ilitenga hizo shilingi bilioni 200, ambazo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kugharamia masuala ya dawa na vifaa na vifaa tiba na vitendanishi. Kiasi cha fedha kilichotolewa mathalani sasa kufikia Aprili, 2021 kimeshabadilika, figure sasa inasoma shilingi bilioni 151.38 na kiasi kilichobaki kama cha shilingi bilioni 50 hivi, tayari tumeshaongea na Wizara ya Fedha, tutapatiwa mwishoni mwa mwezi huu Mei ili tukaendeleo kununua dawa ambazo zilikuwa zimebakia. Kwa hiyo, Serikali itatimiza lengo lake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepokea ushauri na maelekezo ya Kamati katika kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kinga ambapo pia inahusiana na dawa zitakazohusiana na kudhibiti magonjwa mbalimbali eneo hili. Hata hivyo, hali ya upatikanaji dawa muhimu jana nilisema ilifikia asilimia 75, lakini ukweli ukiangalia, suala la upatikanaji wa bidhaa za afya siyo ajenda ya kuongeza bajeti kama nilivyosema. Kama tusipoangalia mambo mapana sana eneo hili hapa tutakuwa kila siku tukiongeza hii bajeti tunajikuta dawa zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya utafiti kwenye Halmashauri zote 184, tumefanya utafiti kwenye hospitali zetu 28 za mkoa, vile vile tumetumia uzoefu ukiwemo wangu mwenyewe nilipokuwa Singida ambapo tulifanya sana mambo haya ya dawa, tumeshirikiana na wadau wetu wote na wataalam wetu wote. Kwa pamoja tumesema lazima tujirekebishe na kujirekebisha huko kuna watu watachukuliwa hatua na wengine wameshachukuliwa, kama *MSD*, 24 wamefukuzwa kazi na wawili wameshushwa mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Halmashauri, katika Hospitali za Mkoa, taarifa tayari imeshakwenda kwenye vyomba vya sheria kwa ajili ya kuwachukulia hatua. Hii ni kwa sababu kuna uzembe mkubwa sana tena hapa ni wa hatari, nimeuambatisha kwenye kiambatisho changu cha hotuba niliyoiwasilisha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukishamalizana; yaani tunakwenda sambasamba kwamba waliokutwa na hizi hatia za kuwa wamefanya ubadhirifu, wamepoteza, wamedokoa, vyombo vya sheria tumeshawakibidhi taarifa, wanafanya kazi zao. Hawa ni *PCCB*, watajua wafanye nini. Vile vile mwajiri na waajiri wote wanaohusika, wanachukua hatua zao kwa sababu kuna Sheria za Ajira za Utumishi wa Umma dhidi ya mtu aliyebainika na hayo makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumechukuwa *dimension* nyingine ya kwenda kwenye vyombo vya taaluma, yaani Mabaraza na Bodi; lazima tuulizane kwamba hivi

unakuwaje mwanataaluma ambaye uzingatii taaluma yako? Wengi wanajitetea kwamba ni uchache wa watumishi, lakini tunakuta matatizo kama haya hata kwenye vituo vikubwa ambavyo watumishi *mashallah*, wana nafuu, lakini mtu unamwuliza maswali anashindwa kujitetea. Kwa hiyo, tunataka tushughulike na hili suala zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, kuna *dimension* nyingine, lazima tuwekeze mazingira ya uwekezaji wa viwanda kuwa mazuri. Jana nilisema viwanda vimeongezeka nchini, sasa tunaongelea hesabu; vilikuwa tisa, sasa viko 11; 16 viko kwenye hatua ya ujenzi na 15 vinajengwa. Maana yake nini? Bei ya kununua hizi bidhaa za afya nje ya nchi sasa itakuwa ni ndogo kwa sababu tutakuwa tunanunua hapa ndani. Kwa hiyo, tunaweka mazingira rafiki na mwongozo uko tayari na ndiyo umetufikisha hapo ili hawa wanaowekeza wawekeze hapa nchini na hela yetu hii tunayosema ni ndogo tuitumie vizuri tupate mzigo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaangalia *dimension* ya ajira kwa watumishi, wataalam wanaohusiana na dawa. Ni kweli utakuta kwenye zahanati au kwenye vituo vya afya wataalam wale ni wauguzi tu, hajasomea dawa. Wakati mwingine unaangalia kumbebesha hili tatizo. Kwa hiyo, kwenye ajira nitakazosisema hapa, tunaangalia Wafamasia pamoja na Wafamasia Wasaidizi tuweze kuwaongeza, tuwapeleke kwenye maeneo yale ambayo yana huduma kubwa zaidi ukilinganisha na yale madogo wataweza kuwafanyia *supervision* wale wa chini yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *dimension* ni nyingi, TEHAMA tumeshajitahidi. Tumefunga TEHAMA, nimeeleza kwenye hotuba yangu; tunataka tuziboreshe zaidi kiasi kwamba tukienda kwenye ule mfumo tuone dawa inaishia pale kwa mgonjwa yule. Pia tumeboresha *prescriptions* za dawa kwamba zinakuwa na *leaf* tatu; *leaf* ya kwanza, yaani stakabadhi moja, unapewa wewe mgonjwa uondoke nayo, stakabadhi moja anakaa nayo daktari aliyekuandikia, stakabadhi moja inakaa kwenye dirisha la dawa. Hiyo

stakabadhi inakuwa na simu ya yule mgonjwa. Yule daktari tutamwuliza, wewe uliandika panadol ngapi mwezi huu mpaka kitabu hiki kimeisha chenye *leaf* labda 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tutaona, tutaenda kufanya *reconciliation* na dirishani, tukitaka tutampigia mpaka mgonjwa tujue. Sasa tutashangaa kama daktari ameandika makopo 20, lakini wagonjwa aliowaona ni wagonjwa wanaoweza wakatumia makopo mawili au kopo moja. Mifumo hii midogo midogo iliachwa, leo hii ukienda pale mtu anapewa dawa tu kama njugu hapewi ile risiti na akipewa haendi nayo nyumbani; lakini benki ukienda unaweka hela zako wewe mwenyewe, unapewa na risiti upeleke nyumbani kwenu ushahidi. Tunataka tuurudishe ule mfumo wa *control and cheques* ili tuanze kulinda hizi rasilimali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *dimension* nyingine ambayo ningependa kuiongelea hapa, suala la kununua dawa, tunaratibu utekelezaji wa mwongozo wa *cost sharing*; yaani ni kwamba zamani tulikuwa na mwongozo lakini sasa hivi tumeuboresha. Ni kwamba utakuwa ukinunua hizi dawa, tunawezesha ile *revolving* yake iweze kuonekana. Zamani tulikuwa tunasema asilimia 67 tunazoweza kuzitumia kwenye eneo la dawa, lakini watu wanakuja wanakwenda chini ya hapo; *data* zinatunyeshwa mtu anatumia asilimia chini ya asilimia 50 (*less than 50*) hata asilimia 25. Ameletewa bidhaa za dawa, akawapatia wateja, wakachangia pesa, lakini hakurudisha kwenda kununua *dawa, definitely* mtaji uta-*Collapse*, kwa sababu inatakiwa iwe *revolved*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukajiuliza huwezi ku-*revolve* dawa peke yake, lazima uende kwenye *dimension ya quality care*; uboresha huduma ili wateja wanaokuja pale pia wawe akina sisi ambao tukiugua na kadi zetu za bima, tunaamua kwenda hospitali zile za akina fulani badala ya kwenda zile za kwetu. Kwa sababu ukienda pale unajibiwa vibaya, mazingira mabovu, hupendelei. Kwa hiyo, tunakuwa tunapata watu wa msamaha kama wale niliowasilisha *data* jana kwamba kwenye *Regional Referral Hospital* shilingi bilioni

nne, kwenye hospitali zetu kubwa za kibingwa, shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni *barriers* za *management system*.zinazosababisha hata huo mtaji wa dawa ukija unaenda kuwapatia watu wasio na bima, kwa sababu wenye bima wameondoka, bima inakuwa inakwenda kwenye vituo vingine na kwenye Serikali hamna kitu; lakini tuna watumishi wetu badala ya kufanya kazi kwenye vituo vyetu na wenyewe wanaondoka, wanakwenda kule *private*. Kwa hiyo, kuna vurugu nyingi sana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, niwape moyo kwamba tumedhamiria kuboresha eneo hili hapa kwa kuangalia *determinants* zote zinazosababisha mtaji wa dawa uyumbe ili tuondoke kwenye dhana ya kwamba Hazina ziko pesa, tutaongeza, tutaongeza; tuweze kufanya *revolving* kwa kutumia fursa ambazo wenzetu wa *private* wanafanya na wanaweza kulipa maji, majengo, mishahara, *promotion* bila kelele kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ili yatekelezeke na yasiwe hadithi, tumeamua kufungamanisha kwenye mikataba ya uwajibikaji kwamba sasa tutageuza sasa hizi ziwe *Score Card Performance Criteria* ili huyu anayepewa kazi hiyo aweze kutekeleza na kupimwa. Hata hivyo tunajuliza, hizi dawa zinapotelea kule kwenye Halmashauri, *determinant* gani nyingine tumeiacha? Ni elimu. Tumefurahi sana kuona leo Wabunge wanaongelea habari ya dawa na wanakiri wenyewe kwamba kweli zinaibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kule Halmashauri tuna mageti yote ya ulinzi, tuna Kamati ya Huduma za Jamii, tuna Kamati ya Mipango na Fedha ya Baraza la Madiwani, tuna Bodi zetu na tuna Kamati za vituo. Huenda hawaelewi. Ripoti zikiletwa hawawezi kugundua viashiria vya upotevu wa dawa au ubadhirifu. Tutawapa elimu hawa wakiwemo Wabunge ambao pia ni Madiwani, wataweza kuwa na

uwezo wa kubaini nini kinaendelea hapa na kuchukuwa hatua kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye madeni yote ya dawa. Ilitolewa hoja hapa kwamba, kwa nini yasifutwe na Wizara ya Fedha? Serikali imeendelea kulipa madeni kwa kadri yanavyohakikiwa ambapo hadi mwezi Aprili, 2021 imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 16.3 na hivyo kubaki kiasi cha shilingi bilioni 260.7. Kati ya deni hilo, shilingi bilioni 31.9 ni deni la vituo vya kutolea huduma za afya na shilingi bilioni 228.7 linatokana na utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya za miradi misonge. Serikali haijafikia utaratibu wa kulifuta hilo deni, lakini imedhamiria kuendelea kulipa deni hilo ili kuiboresha bohari ya dawa (*MSD*) iweze kuimarisha mtaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba niseme mbele ya Bunge lako Tufufu kwamba madeni haya yatalipwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na imeshaanza, lakini tumeweka utaratibu mzuri, vituo vyetu vinadaiwa visinyimwe dawa kule *MSD*. Kuna makubaliano tu wanawekeana pale, wanakuwa wanazichukuwa zile dawa ili na wenyewe wajenge uwajibikaji wa kwenda kusimamia hiyo rasilimali kama nilivyosema. Usipofanya hivyo, unakuta mtu anakosea fomu ya bima, takribani shilingi bilioni 2.4 hazijalipwa na bima kwa sababu walipohudumia wateja wa bima badala wajaze vizuri ili hizo hela zikalipwe kule, wakakosea halafu hawakuulizana hata kuulizana kwa nini tumekosea, tujirekebishe wapi? Ikawa ni mtindo, ni *trend* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka na wao tuwafundishe kwamba watakuwa wanalipa kidogo kidogo bila kunyimwa dawa, lakini waende kwenye uwajibikaji uliotukuka kuangalia *determinants* zote hizi ili kesho tuwe na uongozi wenye ubunifu katika kusimamia rasilimali za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha Simiyu *Medical Product* kuna hoja ilitolewa hapa. Hoja hii imeshafanyiwa kazi na tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha uanzishaji wa kiwanda kitakachozalisha bidhaa

zitakazotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya zinazotumia malighafi yetu ya Tanzania yaani pamba. Serikali kupitia Hazina inakamilisha taratibu muhimu kabla ya kuanza ujenzi wa kiwanda husika Mkoani Simiyu. Tualisimamia hili kwa sababu mifuko iliyokuwa inafadhili imekubaliana na imeshawekana sawa, sasa ilikuwa ni utaratibu tu ya kwamba hizo hela zitakapotolewa zitaweza vipi ku-*revolve*. Hili tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ushauri kuhusu mifumo ya kieletroniki; nimesema hii tutahakikisha tunaiimarisha sana katika vituo vyetu, hivi sasa ngazi ya Taifa vituo saba vinatumia mifumo ya TEHAMA maana ni vituo vyote; kwa ngazi ya mikoa vituo 14 kati ya 28 vinatumia mifumo ya TEHAMA; katika ngazi ya huduma ya msingi, Halmashauri vituo 971 kati ya 7,279 vinatumia hiyo mifumo. Kwa sababu tumeanza kutengeneza mifumo hii kwa wataalam wetu wa ndani, itakuwa rahisi sana kuipeleka kule kwa kasi kubwa katika kipindi hiki ili tuweze kuboresha ufuatiliaji wa taarifa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kidogo niongelee kuhusu masuala mazima ya rasilimali watu. Katika upande wa rasilimali watu, kulikuwa na hoja kwamba kuwepo na mkakati wa makusudi wa kuajiri watumishi wa sekta ya afya na Serikali hususani Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, ihakikishe inatoa vibali vya ajira kwa watumishi wa afya hasa ikizingatiwa kuwa kuna wataalam wengi mtaani. Ndiyo kuna wataalam wengi mtaani ambao tumewasomesha wenyewe lakini hatujaweza kuwapatia kazi na ni wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumejiongeza. Pamoja na kuajiri watumishi wapya kila mwaka, idadi yao kweli bado haikidhi kama nilivyosema. Kwa hiyo, sasa hivi tuna hivi vituo vyetu ambavyo havifanyi kazi. Tuna wastani wa watumishi 2,800 wanastaafu kila mwaka ambapo tumekuwa hatufanyi *replacement* kwa kasi. Kama mliyosikia leo hapa Mheshimiwa Mbunge wetu mmoja alichangia kwamba kumetokea matangazo ya kazi, tuna nafasi takribani 3,337



ukijkumlisha za Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambapo hizi ni *replacement*, ndiyo zimetangazwa na ndiyo tunaendelea kuzifanyia kazi ili kusukuma upatikanaji wa watumishi walioajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kibali chetu cha ajira 2021 maombi ya kibali cha ajira mpya ili kuajiri jumla ya watumishi 13.3 pamoja na kibali cha ajira mbadala hiki nilichokisema sasa hivi, kimetolewa ili kuziba nafasi hizo. Tukaona kwamba hapana, tusiendeleo tu kwenye kutegemea kuajiri, lazima tujiongeze, tufanyeje ili kuongeza *speed* ya wenzetu ambao hawana kazi waweze kupata kazi? Tumetayarisha mwongozo, upo kwenye mapitio ya mwisho katika vyombo vyetu Serikali ili tuweze kuwaajiri watumishi wetu kwa mikataba wakati tunasubiri ile ajira kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ule ukipita, tutaweza kumchukuwa mtumishi tukamwajiri kwa mkataba na anaweza akalipwa nusu ya mshahara wa mtu aliyeajiriwa kama mapendekezo yatapita, kwa hiyo, tutaweza kuwawatia moyo wasikae nyumbani kupoteza ujuzi walionao, wawepo na sisi kadri Serikali inavyopata uwezo, tunazidi kuwachukuwa. Uwezo huo wa kuajiri asilimia 100 lazima tukubaliane tu ni changamoto, siyo tu Tanzania, ni kote kule. Sijui ni wapi walishafika asilimia 100, kwa sababu tunazaliwa kwa asilimia 2.7 kwa mwaka, yaani ni kama vile watu milioni tatu. Unatengeneza hospitali tatu za mikoa, zinazohitaji ikama ya watu 600; sasa, hapa lazima tukubali kuja na huu ubunifu ili tuweze kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika mustakabali mzima wa kukuza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumegundua kwamba ukiacha suala la ajira lazima pia hapa tuangalie *dimension ya productivity*. Unakuta tunao watumishi, ukienda kufuatilia *productivity* yao ipo chini, au sehemu nyingine wako wengi sana, sehemu nyingine wako wachache sana. Wamekaa kwenye maeneo ya mijini; unakuta wako wengi kwa namba au *skills* pale ziko nyingi. Tunafanya *assessment*, tunaitaga WISN, ambayo ni *Workload Indicator of Staffing Needs* ili tuone wingi wa kazi pale walipo ili tuweze kuwasambaza kwenda

kwenye maeneo mengine ambayo yana uhitaji mkubwa kuliko hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunaiita *redistribution*, ilifanyika katika mikoa 11 ambapo ilisaidia kuwapeleka watumishi kwenye ngazi za zahanati na vituo vya afya na maeneo mengine yenye uhitaji. Mikoa iliyotumia mfumo huu ni pamoja na Iringa, Pwani, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Dodoma, Morogoro, Ruvuma, Songwe Mara na Lindi; na tunaendelea.

Naomba nigusie hoja ya *CAG*. Ilitolewa kwamba ripoti ya *CAG* imebaini kuna changamoto katika ununuzi na uendeshaji wa mtambo wa kuzalisha barakoa *MSD* na je, Serikali ina maelezo gani kuhusiana na suala hili? Nimefanya ufuatiliaji, tumefanya ufuatiliaji pamoja na wenzangu wote na taarifa ifuatayo naomba kuiwasilisha kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya upatikanji wa barakoa nchini na duniani wakati wa janga lilipokuwa kwenye kasi kubwa *Covid* 19 Serikali kupitia bohari ya dawa (*MSD*) iliamua kununua kwa dharura mtambo wa kuzalisha barakoa wenye thamani ya dola za Kimarekani 108,700. Mtambo huo ulianza kufanya kazi mwezi Agosti, 2020 ambapo uwezo mtambo huo wakati huo ilikuwa ni kuzalisha barakoa 48,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo ulipoanza kufanya kazi ilibainika kuwa *compressory* ilikuwa na uwezo mdogo wa kufanya kazi, hivyo watumishi walipatiwa mafunzo ya kutumia mtambo huo ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Hivyo, baadaye, baada ya *compressor* hiyo kuwa imeshanunuliwa uzalishaji katika miezi mitatu ya mwanzo, Agosti, Septemba, ni kweli ulikuwa mdogo lakini baadaye ulipanda kwa 148,000 kwa siku. Kutokana na uwekezaji wa mahitaji ya barakoa kwa vituo vya kutolea huduma za afya sasa vituo hivi vinapata pale *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu maneno machache kwamba, sisi kama nchi, masuala haya ya

barakoa, masuala ya *gloves, gowns, protective gear*, ni lazima tufike mahali tujihami sisi wenyewe. Hivi ni vitu vya dharura, vinahitajika *ICU*, vinahitajika kwenye dharura zetu zote zingine zile za majanga, tuna matishio ya *Ebola*, tuna matishio ya vipindupindu na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ilikuwa ni sawa na tija kufanya haya maamuzi ili ile inunuliwe iweze kufanya kazi pale. Hata huko tunakokwenda, huenda tukanunua hata mitambo mingine ya kufanya ulinzi wa wataalam wetu, maana ukitegemea nje katika nyakati kama hizi ndipo unapouziwa barakoa moja shilingi 100,000 unaanza kutengeneza hoja nyingine tena, ilikuwaje, zile hela zinakuwa hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba ieleweke tu kwamba taarifa sahihi ni kama nilivyotoa. Huo mtambo *capacity* yake kwa sasa ni hiyo na ulikuwa ni muhimu na tunahitaji mitambo kama hiyo ili ulinzi wetu katika eneo la afya uwe mzuri zaidi badala ya kutegemea nje ambako zikija tena tunasema hazina viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu miradi ya ujenzi. Miradi ya ujenzi tunayo mingi, niliripoti jana miradi 22 kwenye Kiambatisho Na. 14. Hapa ilitolewa hoja kwamba kule Katavi mkandarasi hayuko *site* licha ya kwamba alitakiwa akabidhi mradi Januari, 2021; kule Hospitali ya Mkoa wa Simiyu nako anasuasua; mradi wa Tumbi nao, *EMD* nao hauko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi unatekelezwa na Mkandarasi SUMA – JKT. Baada ya kuufuatilia na kuona changamoto zake ambazo zilifanyiwa kazi ikapelekea mpaka kubadilisha *consultant*, nimekaa kikao mimi mwenyewe na SUMA – JKT na wale maafande wote tukakubaliana kwamba mradi huo wa Katavi lazima ukamilike kwa wakati. Tunahama kutoka kwenye *conventional contracting* tunakwenda kwenye *force account*, maana tumeona kule ndiyo kuna tija tutaweza kusimamia ukilinganisha na utaratibu uliotumika mwanzo ili

tuweze kwenda na wakati, ifikapo Desemba au mapema Januari mwakani mradi huu uwe umekamilika uanze kutoa huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Tumbi ulikuwa na matatizo, nilitoa maelekezo kwamba ufanyiwe ukaguzi wa kina, kwa sababu ni hatari sana kuja kufikia mahali umemaliza mradi halafu ukakuta kuna tatizo. Taarifa RAS ameifanya, ameikamilisha ataleta na hela zao, bilioni tatu, zipo, tutaziomba zitoke ziende kumaliza kulingana na ile taarifa imesemaje. Hatuwezi kuishia tulipoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kifupi miradi yote hii ambayo inaleta changamoto na sisi tumeamua kupambana na hizo changamoto, ikibidi kwa ku-*review* ile mikataba tuweze kwenda kwenye *force account* ku-*accelerate speed* ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala kuhusu kumaliza Wodi ya Saratani Bugando. Hii Wodi ya Saratani Bugando ni muhimu sana, tena itapunguza msongamano sana katika Hospitali yetu ya *Ocean Road*, lakini itawapunguzia wananchi mzigo wa kwenda *Ocean Road*, kuhama na ndugu zao waje, gharama zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetenga fedha kwenye mwaka huu ambazo ni kama bilioni 1.8, tutazitoa. Tutaangalia kama tutaweza kwenda na kasi ya kumaliza hizo hela kwa wakati ili hela isilale ili tuweze kufanya mpango kupitia Kamati yetu ya Bajeti. Ni suala la kuomba tu kibali kwamba hawa wamekwenda na kasi inayotakiwa tuweze kuona namna gani tutafanya *reallocation* ndani ya Fungu la Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Afya kuweza kuhakikisha ile wodi inakamilika. Maana vinginevyo, kama hatutafanya hivyo, tunaendelea kuwaumiza hawa wananchi na kuendelea kuiumiza *Ocean Road* kwa wagonjwa ambao wangeweza wakatibiwa huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali yetu ya Kwangwa iliyoko Mara kwamba ikamilishwe mapema, kwani

ikikamilika inamuenzi Hayati Mwalimu Nyerere. Ni kweli, Wizara imedhamiria kukamilisha hospitali hii. Inajengwa kwa jengo moja ambalo lina vitalu vitatu; Kitalu A, Kitalu B na Kitalu C. Kwa sasa jengo la Kitalu C limekamilika na huduma za afya ya mama na mtoto zinaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetenga bilioni 11 katika bajeti ya fedha ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Hospitali ya Mkoa wa Mara, Kitalu A na Kitalu B, ujenzi wa jengo la kuhifadha maiti, jengo la kufulia na kuboresha mazingira yanayozunguka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, kwa hiyo tuko *serious* kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wangu umekwisha, nimalizie tu neno moja kuhusu madirisha mangapi ya kutolea huduma kwa wazee. Tuko *serious* na wazee; kama juzi tulipokuwa na Mheshimiwa Rais niliweza kusema kwamba tumekwenda mbele, tumefanya kikao na mitandao inayoratibu shughuli za wazee ambayo ni taasisi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba madirisha ta wazee yasiwe tatizo. Tumekwenda kuteua watu watatu kila kituo; Muuguzi yupo, Daktari yupo na Nesi yupo, hawa tutawavalisha ma-*T-shirt* yanaitwa Nakupenda Sana Mzee. Watakuwa wakifika pale hata kama watumishi ni wachache hakuna dirisha maalum, apokelewe kama *VIP*, apelekwe kwenye chumba ambacho kitamuona huyu mzee. Mwenyekiti wa hii shughuli ni mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tayari wataalam wangu wameshakusanya haya majina na *numbers* zipo kule, mdogomdogo tumeshaanza. Sisi wenyewe ni wazee watarajiwa, tupende kukutana na mambo ambayo tulijiandalia sisi wenyewe huku wakati tukiwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Wazee tunaifanyia mapitio ili ije kuwa sheria ambayo itatambua haki zao kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha hoja na yote mengine yaliyosemwa sisi tumeyapokea, wanaoniomba niambatane nao kwenye majimbo yao niko tayari, baada ya Idi tunakwenda wote tukayaone yaliyoko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu; Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, tukae.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 52 – WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management...*, ... ..Sh. 5,647,807,864

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri. Nimeletewa majina hapa ya Wajumbe mbalimbali ambao wanahitaji ufafanuzi. Tutaanza na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa nilizungumza hoja yangu ya hofu yangu ya aina za chanjo na teknolojia iliyo nyuma ya chanjo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikusudia kumwondolea Mheshimiwa Waziri shilingi nisipopata maelezo ya kutosha kwa sababu kuna nchi jirani ambayo siwezi kuitaja kwa sababu ya mahusiano yetu ya kidiplomasia, ambayo watu wake watatu baada ya kuchanjwa tu wamefariki. Kuna nchi nyingine pia ambayo iko Mashariki ya Kati ambayo watu wanakufa sana kwa sasa hivi mpaka wanakosa kuni za kuchomea, lakini taarifa ya Daktari mmoja anaitwa Gupta inaonesha wanaokufa sana ni wale waliochanjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba suala hilo linafanyiwa kazi na maprofesa wetu, naomba nisimwondolee shilingi, nisubiri mpaka taarifa ya maprofesa wetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba ufafanuzi kwenye eneo la Serikali kulichukua deni la *MSD* Serikali kulichukua kwa sababu Waziri wakati ana-*wind up* hapa hakutoa majibu, hajachukulia uzito juu ya ukosefu wa dawa kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa sababu mwaka 2019/2020, ruzuku ya dawa haikutolewa kabisa, mfano kwenye Halmashauri yangu ya *Arusha DC*. Pia Waziri hajaonesha jinsi ambavyo amejizatiti na suala hili, hajaonesha kama yuko *serious* katika suala hili. Kwa nini Serikali isichukue hili deni ikaondoa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za mkoa, badala ya kuendelea kusema italipa kidogokidogo, matokeo yake wananchi wanaendelea kuteseka na vilio na maombolezo kwa akinamama, watoto na wajawazito? Naomba kama hatanijibu vizuri nitashika shilingi ya mshahara wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwombe kaka yangu, Mheshimiwa Lemburis, amuachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake kwa sababu kwanza utaona Mheshimiwa Waziri ameonesha kwanza kilichotokea mwanzoni, kwamba Serikali imetoa fedha nyingi sana kweli kwenye hili eneo la dawa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipokuwa panafanywa *tracing*, maana yake ukitoa dawa nyingi sana kuna *percent* ambazo ni zile zinazokwenda kwa wale wagonjwa ambao wanatibiwa bure, lakini kuna *percent* ambazo zinazuwaa, lakini Serikali ilipokuwa ina-*trace* kwenye mfumo huo hizo dawa ilikuta hazionekani. Ndipo Serikali ikasema ni lazima Wizara ijielekeze ije na sababu ni kwa nini dawa hazionekani kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliunda timu zikaenda mkoa yote, zikaja na zikaonesha fedha ilitokana na nini na kulikuwepo na upotevu wa bilioni 26. Akaunda timu zikaenda wilaya zote na zimekuja na ripoti ambazo ndizo alizosema amekabidhi kwenye vyombo husika. Nafikiri Waheshimiwa wameona hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwahidi Mheshimiwa Lemburis kitu kimoja, kwamba sasa *structure* ambayo tayari Waziri ameshaziainisha kwa maana ya kujifunza mikoani na kujifunza kwenye ripoti zilizoko wilayani kwa bilioni 80 ambazo Rais, mama Samia Suluhu, amezitoa na bilioni 43 ambazo amezitoa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, zitakwenda sasa ku-*capture* kuhakikisha huo mfumo ambao ulikuwa unapoteza dawa hautakuwepo, kwa hiyo dawa zitapatikana kwenye vituo na hata *CHF* itatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane na ukweli mmoja; madeni ambayo yanasemwa *MSD* inadai kwenye vituo vyetu yanatokana na huu ubadhirifu. Nimwombe kaka yangu, vyombo vilifanyie hilo jambo kazi halafu tutarudi hapa, tutakaposhindwa baadaye kutoa majibu, baada ya vyombo vyote kufanya ili kutenda haki, Mheshimiwa atashika shilingi,



lakini kwa leo kwa sababu jambo hilo liko kwenye *process* na *structure* zimeshaainishwa kuhakikisha dawa zote zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameelekeza hapa jinsi, siyo tu tutakwenda kuchunguza dawa iko wapi, lakini tutachunguza kidonge hadi kidonge na ni nani amekunywa, nina hakika dawa zitapatikana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kutuachia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pia namshukuru kidogo Mheshimiwa Waziri, amegusia suala la Wodi Maalum ya Saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo maelezo ya Mheshimiwa Waziri yako kwenye kitabu chake kikubwa, hospitali ile ilianza na kuhudumia wagonjwa 320 kwa mwaka, leo inahudumia takribani wagonjwa 14,000 kwa mwaka. Hata hivyo, katika taarifa mbalimbali inaonesha kwamba asilimia karibu sabini ya wagonjwa wa saratani walioko *Ocean Road* wanatoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mikoa ya Kanda ya Ziwa ina *population* takribani milioni 20 ya *population* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri; mahitaji ya kukamilisha Wodi ya Saratani ili kuepusha rufaa zinazokwenda Bugando ni bilioni tatu tu, lakini sijasikia *commitment*. Amezungumzia jambo ambalo kama vile halieleweki, kama vile litafikiriwa, kama vile halina umuhimu hivi. Nataka *commitment* ya Waziri ya kupatikana bilioni tatu za kukamilisha Wodi ya Saratani ya Bugando. Kama hakuna *commitment*, nashikilia shilingi ya Waziri. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja ikae vizuri kwa sababu swali linapaswa kuwa la kisera na nataka kuelewa vizuri, maana yeye anazungumzia bilioni tatu mahususi kwamba zinahitajika kwenye hiyo hospitali. Sasa tusije tukachanganya mambo

hapa; kwenye bajeti yenu hilo jambo lipo au halipo? Kwa sababu yeye anatakiwa kuuliza swali la jumla, la kisera, kwa hiyo uhitaji wa hizo huduma za wagonjwa wa saratani kwenye hospitali hizo za kanda ama hospitali hizo kubwa, sasa yeye ametaja mfano mahususi kwa sababu anasema kitakwimu wagonjwa wengi wanatokea Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo uhitaji wa hiyo Hospitali ya Bugando kuweza kutoa hiyo huduma kwa hao wagonjwa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kaka yangu, Mheshimiwa Kanyasu, ameuliza swali muhimu sana na tunatambua kwamba pale kwenye Hospitali ya Bugando zinatakiwa hizo bilioni tatu alizotaja ili kumaliza *bunker* kwa ajili ya wagonjwa wa saratani, lakini kwa bajeti hii kuna bilioni 1.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge hili lielewe kila mwaka kwenye Hospitali hiyo ya Bugando, Serikali inapeleka pale bilioni 9.2 kwa ajili ya mishahara. Pamoja na hiyo bilioni 1.8 ambayo sasa kwa bajeti hii imewekwa na imefikiriwa wakimaliza hizo fedha ambazo ni bilioni 1.8 mapema, itafanyika *reallocation* baadaye kwa ajili ya kuwapa hela nyingine kwa mfumo ambao umetolewa na Wizara ya Fedha ili kuweza kumaliza hiyo kazi anayoisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alichokifanya, ameunda vilevile timu, siyo suala la kusema tutengeneze tu *bunker* na kuhakikisha tunawatibu; kuanza kutafuta *source* ni kwa nini wagonjwa wengi wanatokea kwenye hiyo Kanda ya Ziwa ili tuhakikishe kwamba hata kile kinachokuwa *source* ya kutokea ugonjwa tuweze kukijua na kuki-*address*. Kwa hiyo hiyo timu iko vizuri na kazi inafanyika, kwa hiyo suala la Mheshimiwa limekaa kwa mtindo huo, tunamomba amwachie Waziri shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hii bilioni 1.8 ni kwa ajili ya hilo jengo la saratani?

Mheshimiwa Kanyasu, naona umesimama.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa swali lako la msingi. Kwenye maelezo ya kitabu, haiku *specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ujenzi wa jengo hili haujaanza mwaka huu; alialikwa Mheshimiwa Waziri Mkuu akamtuma Waziri wa Afya wa mwaka ule, akaenda kufanya harambee akiwa mgeni rasmi. Watumishi wa Bugando wametoa mishahara yao kuchangia na Serikali imekuwa ikipeleka pesa kidogokidogo. Hata hivyo, Serikali inakiri ongezeko la wagonjwa *Ocean Road* na watu wanakufa. Sasa sijui kwa nini Mheshimiwa analiona suala la kawaida tu...

**MWENYEKITI:** Sawa.

Mheshimiwa Kanyasu, kwenye ngazi hii Waziri amejibu kwamba hizo unazosema bilioni tatu, kwa bajeti hii ya 2021/2022 wametenga bilioni 1.8 kwa ajili ya jengo hilo. Kuna namna yoyote ambayo jengo linaweza likajengwa kwa muda mfupi yaani, au mimi ndiyo sijekuelewa hoja yako. Kwa sababu nilikuwa nakusikiliza, ukisimama kwa kawaida mara ya pili unatoa tu hoja kama unataka kushika shilingi au hapana. Kwa hiyo hoja...

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza tuelewane vizuri; bilioni 1.8 zilizoko kwenye bajeti, wewe unaona hazitoshelezi, ndicho unachotaka kusema, kwa bajeti ya mwaka huu?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hazitoshelezi. Naomba nitoe hoja.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa kama ni hivyo Waheshimiwa Wajumbe, kwa Kanuni zetu ukija kwa namna anavyozungumza hoja yake Mheshimiwa Kanyasu, unatakiwa kueleza hizo fedha za ziada zipatikane vipi, ndivyo Kanuni zetu zinavyosema na ndiyo maana saa ya kushika

mshahara wa Waziri unazungumza jambo la kisera, kwa sababu hapa hupendekezi kipi kinaongezeka, wapi zinapungua. Ukitaka kuongeza fedha zaidi ya bajeti iliyoletwa hapa na Serikali, lazima useme chanzo cha fedha hizo ni kipi.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hilo tumeelewana vizuri. Kwa hiyo hakuna hoja inayoweza kutolewa hapo kutoa shilingi kwa hoja hiyo, nadhani mmenielewa vizuri. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo. Samahani ninakubaliana na maelezo yako, lakini suala hili linagusa Hospitali ya Kanda na Hospitali za Kanda ni suala la kisera na mimi... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu hebu kaa kidogo tuelewane vizuri, tuelewane vizuri. Ni hoja ya kisera Serikali kupeleka fedha huko kwenye hizo hospitali ili huduma itolewe, hiyo ni hoja ya kisera. Hoja ya kwamba bilioni 1.8 hazitoshi kwenye bajeti ijayo siyo hoja ya kisera kwasababu hiyo sasa lazima utuambie hizo fedha za ziada 1.2 zitoke wapi? Ndiyo kanuni zetu zinavyosema, tuzisome kanuni Waheshimiwa Wabunge.

Ndiyo maana nilikuwa nakupeleka vizuri ili ujue hoja yako utaitoa vipi sasa wewe umeitoa hoja kwamba fedha hizo hazitoshelezi, zitoke wapi hizo 1.2 kwasababu Serikali imejipanga kwa ajili ya 1.8. Kwa hiyo, ndiyo maana nilikuwa nakuongoza vizuri lakini sasa umetupeleka huko kwenye kuongeza fedha ambazo hujasema zitatoka wapi. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi Sera yetu ya Afya pamoja na Mipango Mbalimbali ya Taifa na hasa ukizingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 inajielekeza

kutoa huduma bora kwa watu wote kwa maana ya Watanzania wote na kupunguza vifo mbalimbali vinavyotokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano vifo vya Watoto wa chini ya umri wa miaka mitano ni Watoto 312 kila siku wanafariki Tanzania, jua linapochomoza na linapozama Watoto 312 wanafariki. Lakini kuna vifo vinavyotokana na uzazi kati ya vizazi hai 100,000 kuna vifo 435 sasa, sababu ya vifo hivi vinatokana na mambo mengi lakini kubwa ni uduni wa utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Ninahitaji kupata *commitment* ya Serikali na namna gani vifo hivi vinapungua na vinakwenda kuisha kama sitaridhika na majibu ya Serikali nitashika shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze dada yangu kwa kugusia eneo hilo nyeti, ambalo siyo tu nyeti hata kwenye hotuba ya Rais alipokuja Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan alilirudia mara tatu tena aka-*pause* kuonyesha kwamba ni eneo muhimu sana, kwa hiyo kwa kweli ni eneo nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mbunge Mwenzangu ndiyo maana utaona kwa bajeti hii imeongezeka bajeti kutoka bilioni 55 kwenye eneo hilo kwenda bilioni 63. Lakini ukisikia uboreshaji wa vile vituo vya afya ambavyo tunasema ili sasa ifike mahali kule Karatu kwenye kituo cha afya upasuaji uweze kufanyika ndiyo maana unasikia vile vituo zaidi ya 300 ambavyo sasa vinaenda kufanya hilo suala la upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ni kuhakikisha upatikanaji wa dawa, kuhakikisha upatikanaji wa dawa kwamba wakati wote dawa zinapatikana. Lakini ukija kwenye eneo la bima ya afya kwa wote halitakuwa na *effect* sehemu

moja unaposema unakuwa na bima ya afya kwa watu wote maana yake mwisho wa siku unapozungumzia huduma ya wazee bure, huduma ya Watoto bure, huduma ya akinamama bure tayari inakuwa imekuwa *covered*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa *covered* eneo hilo maana yake ni nini, maana yake Serikali itajitoa sasa kwenye eneo la kupeleka fedha za kila siku kwenye vituo vyetu kwasababu vitaweza ku-*rotate* vyenyewe, fedha nyingi sasa zitaenda kwenye *infrastructure* ambazo zile *infrastructures* zitashuka sasa chini ambazo sasa zitaenda kuondoa tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge umeanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuambie Mheshimiwa Roma haikujengwa kwa siku moja. Na sisi kwenye eneo hili la afya unaona *progress* tumetoka kwenye kupeleka asilimia 98 ya watu wanaenda nje, wanaenda kutibiwa nje wenye matatizo yale makubwa leo asilimia 95 wanatibiwa ndani ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwamba sisi ndiyo tunaenda nje kuwatibu watu wetu sasa tuna nchi zaidi ya 18 zinakuja kutibu watu wao hapa Tanzania. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Parreso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sijaadhihika na hiyo *commitment* ya Serikali hivyo nashika shilingi na ninaomba kutoa hoja Wabunge waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Haya hoja haijaungwa mkono.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haa nyie ya  
ani akina mama nyie...

**MWENYEKITI:** Hoja ili iungwe mkono lazima niwaone watu kumi wamesimama, kwa hiyo sijawaona. Jihesabuni

mipo wangapi mliosimama, haya, haya ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Sima. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, nchi yetu ilikumbwa na janga la *Corona* na tumetumia dawa nyingi sana zikiwemo dawa za asili kujikomboa kwenye hii hali lakini pia imekuwa fursa ya kufanyika utafiti wa dawa ambazo zimetusaidia ikiwemo dawa inaitwa *fight exponent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa hii imebahatika kupata semina kwenye kamati yangu ya Huduma za Jamii imeonyesha namna ambavyo inauwezo mkubwa wa kuimarisha kinga ya mwanadamu kwenye magonjwa mbalimbali. Lakini imesajiliwa kama kirutubisho tiba, sasa kuwa kirutubisho tiba maana yake inabaki kwenye eneo la uwasil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka *commitment* ya Serikali na kama Mkemia amethibitisha kwamba inafaa kuwa dawa, dawa ambayo inaweza kuwasaidia watu wote kwenye mambo mengine, nahitaji *commitment* ya Serikali kwa nini sasa tusitumie fursa hii kwenye dawa hizi ambazo zimefanyiwa utafiti na mkemia amekubali ziwe dawa kamili ambazo hazitakuwa na kodi na zitatolewa kwa gharama nafuu kila mtanzania aweze ku-*afford*. Nilikuwa nataka tu hili, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hoja hii, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuhakikisha kwamba anabidhaa ambayo kweli inaweza ikajibu matatizo yetu sisi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nalifahamu na nimekuwa nikilifuatilia sana mimi mwenyewe kwamba basi kama limeshatoka kwa mkemia wa Serikali kwamba ni

salama inaweza ikatumika, inakuwa *categorized* kwamba ni nini, hii imekuwa *categorized* kama *food supplement*. Hatua inayofuata ili tuende kuwa na dawa tunayoitumia lazima *TFDA* au *TMDA* taasisi yetu ile, ya *TMDA* ipate wasilisho la ku-*submit* kwake ili na wenyewe wafanye kazi yao kisheria, wakishamaliza wale tu hii tayari sisi tunaitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasiliana jana katika kikao changu cha kujiandaa na masuala haya Mkurugenzi wa *TMDA* anasema hajapokea hata hizo *submission* za kuomba ifanyiwe kazi na *TMDA*. Kwa hiyo, *commitment* yangu ni kwamba mara baada ya Bunge hili leo nitoke naye mguu kwa mguu akanipe vielelezo nimpeleke *TMDA* yupo Ofisini kwangu ananisubiri. Tumalize tupone. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sima ameridhika. Lakini ni kweli Mheshimiwa Waziri hata mimi nimesikia hadithi nyingi kuhusu watu waliotumia hii dawa, kuna wale ambao walipata athari kubwa za *Covid* wale ambao inabidi sasa atoke na *machine* kabisa hospitali ya kuanza kutumia.

Lakini baada ya kufika nyumbani wiki kadhaa basi ametumia hiyo kidogo anaweza akatoa kidogo akaweka tena, akatoa kidogo akaweka tena, kwa hiyo, nadhani ni dawa ambayo inaweza ikatusaidia kwenye mambo mengi badala ya kutumia gharama kubwa sana kuwatibu wagonjwa wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo Wabunge waliokuwa wanataka ufafanuzi, sasa kwa muda wetu uliobaki hapo kanuni inatutaka tuende kwenye *guillotine*. (*Makofi*)

Katibu!

**FUNGU 52 – WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA  
WAZEE NA WATOTO**

Kifungu 1001- *Administration Human  
Resources Management*.....Sh.5,647,807,864



Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> . . . . .	Sh.1,751,394,520
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i> . . . . .	Sh.1,597,108,016
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> . . . . .	Sh. 552,500,447
Kifungu 1005 - <i>Government Communication Unit</i> . . . . .	Sh. 293,069,000
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i> . . . . .	Sh.1,047,971,660
Kifungu 1007 - <i>Legal Service Unit</i> . . . . .	Sh. 363,902,029
Kifungu 1008 - <i>Information and Communication Technology Unit</i> . . . . .	Sh. 727,113,415
Kifungu 2001 - <i>Curative Services</i> . . . . .	Sh. 444,628,506,226
Kifungu 2003 - <i>Chief Medical Officer</i> . . . . .	Sh. 45,228,293,278
Kifungu 2004 - <i>Nursing and Midwifery Services Division</i> . . . . .	Sh. 660,770,253
Kifungu 2005 - <i>Pharmaceutical Services Unit</i> . . . . .	Sh.1,114,544,000
Kifungu 3001 - <i>Preventive Services Delivery</i> . . . . .	Sh. 24,755,787,467
Kifungu 3002 - <i>Health Quality Assurance Division</i> . . . . .	Sh. 696,349,984
Kifungu 3003 - <i>Health Emergence Preparedness Response Unit</i> . . . . .	Sh. 290,670,000
Kifungu 4002 - <i>Social Welfare</i> . . . . .	Sh. 62,000,000
Kifungu 5001 - <i>Human Resources Development</i> . . . . .	Sh. 27,885,270,841
Kifungu 6001 - <i>Amana Regional Referrals Hosp. DSM</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6002 - <i>Bombo Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6003 - <i>Dodoma Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh . 0
Kifungu 6004 - <i>Geita Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6005 - <i>Iringa Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6006 - <i>Kagera Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh . 0
Kifungu 6007 - <i>Katavi Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6008 - <i>Ligula Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6009 - <i>Manyara Regional Referrals Hosp.</i> . . . . .	Sh . 0
Kifungu 6010 - <i>Mara Regional Referrals Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6011 - <i>Maweni Regional Ref. Hosp. - Kigoma</i> . . . . .	Sh . 0
Kifungu 6012 - <i>Mawenzi Reg.Ref. Hosp. - Kilimanjaro</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6013 - <i>Mbeya Regional Ref. Hospital</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6014 - <i>Morogoro Regional Ref. Hosp.</i> . . . . .	Sh. 0
Kifungu 6015 - <i>Mount Meru Reg. Ref. Hosp. - Arusha</i> . . . . .	Sh 0
Kifungu 6016 - <i>Mwananyamala Reg. Ref. Hosp. - DSM</i> . . . . .	Sh. 0

Kifungu 6017 - Njombe Reg. Refferals Hosp. ....	Sh. 0
Kifungu 6018 – Sekou Toure Reg. Ref. Hosp. Mwanza.....	Sh. 0
Kifungu 6019 - Shinyanga Regional Referrals Hospital.....	Sh. 0
Kifungu 6020 - Simiyu Regional Referrals Hospital ....	Sh. 0
Kifungu 6021 – Singida Regional Referrals Hospital ....	Sh. 0
Kifungu 6022 - Sokoine Reg. Ref. Hosp.- Lindi ....	Sh. 0
Kifungu 6023 - Songea Reg. Ref. Hosp. - Ruvuma ....	Sh. 0
Kifungu 6024 – Songwe Regional Referrals Hospital ....	Sh. 0
Kifungu 6025- Sumbawanga Reg. Ref. Hosp.- Rukwa.....	Sh. 0
Kifungu 6026 - Tabora Regional Referrals Hospital ....	Sh. 0
Kifungu 6027 - Temeke Reg. Ref. Hosp. - DSM ....	Sh. 0
Kifungu 6028 - Tumbi Reg. Ref. Hosp. - Pwani ....	Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **FUNGU 53 - WIZARA YA AFYA, IDARA KUU MAENDELEO YA JAMII**

Kifungu 1001- <i>Administration and Human Resource Management</i> ....	Sh. 1,457,037,400
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ....	Sh. 506,794,800
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i> ....	Sh. 620,876,000
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 267,712,000
Kifungu 1005 - <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 232,995,000
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 352,275,000
Kifungu 1007 - <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 226,614,000
Kifungu 1008 - <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh. 204,302,000
Kifungu 2001 – <i>Community Dev. Institutes</i> ...	Sh.10,657,508,000
Kifungu 2002 – <i>Community Development</i> ....	Sh. 887,780,800
Kifungu 2004 - <i>Nursing and Midwifery Services Division</i> ....	Sh. 660,770,253
Kifungu 2005 - <i>Pharmaceutical Services Unit</i> .....	Sh.1,114,544,000
Kifungu 3001 – <i>Gender Development</i> .....	Sh. 700,591,000
Kifungu 3002 – <i>Children Development</i> ....	Sh. 691,029,000

Kifungu 4001 – <i>Non-Government Organization...</i>	Sh.1,206,276,000
Kifungu 5001 - <i>Social Welfare Division</i>	Sh.10,712,138,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO MAENDELEO

### FUNGU 52 – WIZARA YA AFYA IDARA KUU - AFYA

Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 7,258,993,827
Kifungu 2001 - <i>Curative Services</i>	Sh.114,493,909,863
Kifungu 2003 - <i>Chief Medical Officer</i>	Sh. 0
Kifungu 2005 - <i>Pharmaceutical Services Unit...</i>	Sh. 218,100,000,000
Kifungu 3001 - <i>Preventive Services Delivery...</i>	Sh. 476,830,236,000
Kifungu 3003 - <i>Health Emergence Preparedness Response Unit</i>	Sh.120,000,000
Kifungu 5001 - <i>Human Resources Development</i>	Sh.11,150,473,636

*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 53 – WIZARA YA AFYA, IDARA KUU MAENDELEO YA JAMII

Kifungu 2002 – <i>Community Development</i>	Sh. 3,600,000,000
Kifungu 3001 – <i>Gender Development</i>	Sh.1,436,989,380
Kifungu 3002 – <i>Children Development</i>	Sh.616,994,000
Kifungu 5001 - <i>Social Welfare Division</i>	Sh. 9,246,017,620

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Mtoa hoja, taarifa!

## T A A R I F A

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Namba 123(3)(a) na (b) naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
(Hoja liliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022 waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo, nafikiri walioafiki wameshinda.  
*(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru kwa uamuzi huo mlioufanya siku ya leo wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na pia nichukue fursa hii kwa niaba

yenu nyote kuwapongeza sana, Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wawili, wanaomsaidia kazi na watendaji kazi wake, tunawapongeza kwamba yale maombi mliyokuwa mmeyaleta Bunge limewapitishia. *(Makofi)*

Sasa tunawatakia kila la heri katika yale yote mliyoahidi kwamba, mtayafanyia kazi yapo yale ambayo mmeyaahidi kwenye bajeti, lakini yapo mambo ambayo mtayafanyia kazi kwa maana ya utekelezaji namna ya kutekeleza vizuri zaidi mawazo ya Wabunge yaliyotolewa ni mengi, mkayafanyie kazi na yale ambayo hayakuwepo kabisa katika mpango wenu wa mwaka huu wa fedha unaokuja basi mtazame kwa huko mbele yale marekebisho ambayo yanahitajika ili wananchi wetu wawe na afya bora kabisa.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji tukiamini kwamba mtayafanyia kazi yale ambayo mmetuahidi na Bunge limewaamini kwa kuwaidhinishia hizo fedha mlizoomba.

Waheshimiwa Wabunge nichukue fursa hii, kuwatakia kila mmoja wenu kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na Uongozi wote wa Bunge, tunawatakia Idd njema, tunawatakia Idd njema, tunaamini yale matendo mema ambayo yalikuwa yakitendeka, ilianza Kwaresma, ikaja Ramadhani, tunaamini yataendelea kwa mwaka mzima mpaka mwakani tena, tutakapokutana na Kwaresma na Ramadhani. Tusiwe tunafanya tu matendo mema kipindi hiki na hata ikiwa ni pamoja na yale matendo ya kualikana kwenye futari na mambo kama hayo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya tarehe 17 Mei, 2021 siku ya Jumatatu saa tatu kamili Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 06.56 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 17 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*